# Nipashe

Jumamosi Machi 26, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580896

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



SportPesa
TZS. 1,065,872,000
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Mwanamke** apambana na mbweha, amuua

UKURASA 2



**PEDRI AMUITA HAALAND BARCELONA**

UKURASA 22



# Vigogo wapeana maeneo ya jeshi

• **Rais** Samia aanika kila kitu, agoma kutoa ajira mpya Magereza kisa... *Endelea ukurasa 2*

RIPOTI MAALUM- 2

## Ushuhuda vifo vya wavuvi uchafuzi wa Mto Mara

UKURASA 4



Mwenyekiti wa **CHADEMA**, Freeman Mbowe.



Mwenyekiti wa **CHAUMMA**, Hashim Rungwe.



Kiongozi Mkuu wa **ACT-Wazalendo**, Zitto Kabwe.



Mkurugenzi Mtendaji wa **LHRC**, Anna Henga.

## Mbowe na wenzake washinda kesi Sheria Vyama vya Siasa

UKURASA 2


**MICHEZO** **WACHEZAJI SITA MTEGONI SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Mwanamke apambana na mbweha hadi kumuua

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji na Kata ya Mkoka, Liwale mkoani Lindi, Zuwena Mandale (42), ameibuka kuwa shujaa wa kuokoa usalama wa maisha yake baada ya kupambana na mbweha aliyekuwa amemvamia na hatimaye kumuua.

Mnyama huyo alimvamia mwanamama huyo mwilini na kumshambulia kifuani na hatimaye kupata nafasi ya kujiokoa na kumkatakata mapanga kichwani.

Taarifa kutoka kijijini hapo ya kuthibitishwa na mhusika mwenyewe na Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Agnes Thomas, zinaeleza kuwa tukio hilo limetokea Machi 20, mwaka huu, alasiri wakati Mandale akiwa njiani kutoka shambani kurejea nyumbani.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii, Mandale alisema siku hiyo akiwa njiani kutoka shambani, alivamiwa na mbweha huyo aliyekuwa mbele yake na kumng'ata kidole gumba cha mkono wa kulia na kumsababishia majeraha yaliyoambatana na maumivu makali.

Mandale alisema baada ya hapo, mnyama huyo alimrukia kifuani lakini alifanikiwa kujiokoa na kupambana naye hatimaye kumwangusha chini na kumkandamiza huku akipiga kelele kuomba msaada kwa wapita njia.

Hata hivyo, alisema mmoja wa wanaume aliyekuwa karibu na tukio hilo, alishindwa kumpa msaada kwa madai alikuwa anamwogopa mnyama huyo.

Alisema baada ya kuelezwa hayo, aliendelea kupambana huku akimkata mapanga kichwani na hatimaye kumuua mbweha huyo.

Mwanamke huyo alisema wakati akiendelea kupambana na mbweha huyo, mwanamume mwingine aliyemtaja kwa jina la Tindo, alifika eneo la tukio kumsaidia lakini tayari alikwisha kumuua kupitia panga alilokuwa nalo.

Ofisa Mtendaji Kijiji, Agnes Thomas, alithibitisha Mandale kushambuliwa na mbweha huyo na kung'atwa kidole gumba cha mkono lakini alifanikiwa kujiokoa na kumuua. Baada ya hapo alipelekwa Kituo cha Afya Mkoka kwa ajili ya matibabu.

Thomas aliwasisitiza wananchi kuweka mazingira ya usafi maeneo yanayozunguka nyumba zao kwa kuondoa nyasi na vichaka kwa kuwa wanyama na wadudu wanatumia mwanya huo kufika hadi kwenye makazi hayo.

# Vigogo wapeana maeneo ya jeshi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema uvamizi wa maeneo ya Jeshi la Magereza unafanywa na maofisa wenyewe kutokana na kupeana kama zawadi wakati wanapostaafu.

Pia amesema hakusudii kutoa ajira mpya kwa jeshi hilo kwa sasa na kuagiza askari waliopandishwa vyeo, wasio na ofisi warudi kusimamia wafungwa.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizindua na kuweka jiwe la msingi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ya jeshi hilo.

"Hili suala la maeneo kuvamiwa nalitupa kwenu kwa sababu Magereza mna ardhi kubwa lakini kutokuitumia ndiko kunatoa fursa ya wananchi kuvamia.

"Lingine ni ninyi wenyewe mkishastaafu mnakatiana maeneo. Watu wakiona wengine wanajenga kwa nini wao wasivamie? Kwa hiyo naomba sana mtunze maeneo yenu wenyewe na kama mnapeana zawadi ya maeneo basi tengeni eneo hili wastaafu wetu wakitoka ndilo eneo la zawadi," alisema.

AKATAA OMBI LA AJIRA

Kuhusu ajira, Rais alikataa ombi la Kamishna Jenerali wa Magereza la kuajiri askari wengine kutokana na wengi kupandishwa vyeo, hivyo kusababisha upungufu kwenye usimamizi wa wafungwa.

"Hawa wengi nimewapandisha vyeo kwa mapendekezo kutoka kwenu na mimi nilijua mkipendekeza hawa wapandishwe vyeo wanakwenda kufanya kazi zipi? Haina maana mtu akiwa na cheo aende kukaa ofisini hana kazi. Kama wamepandishwa vyeo kwa wingi huo nina hakika kuna watu wanazurura kwenye korido za ofisi hawana kazi, warudi wakasimamie wafungwa.

"Hatuwezi kuajiri kila mwaka. Sasa kama una cheo huna kazi ya kufanya rudi kafanye kazi yako, cheo chako utabaki nacho wala hakiondoki. Wanasema waridi ni waridi na harufu ni ile ile, kama ulifikia cheo gani cheo chako ni hicho hicho hata kama unakwenda kusimamia wafungwa ni hicho hicho. Msitulazimishe kuajiri watu wapya kwa sababu watu wengi wamepanda vyeo, vinginevyo mtanifanya nisipandishe.

"Niombe sana hili la ajira sitatoa. Nimezungumza kwa siri na Kamishna wa Magereza ameomba niajiri askari hata kama wa darasa la saba wakasimamie wafungwa. Kusimamia wafungwa kunataka uzoefu inataka mtu aliyepata mafunzo mazuri. Wale niliowapandisha vyeo ndio wana uzoefu wa kusimamia wafungwa, warudi kuwasimamia na sitatoa kwa sasa ajira mpya," alisema.

Akizungumza kuhusu majeshi kukimbilia uzalishaji mali, alisema mwelekeo wa sasa majeshi yanakwenda kuacha kazi zao wanazotakiwa kuzifanya na kukimbilia huko.

"Tukiendelea hivi tutajikuta kweli tunazalisha zaidi lakini zile nyanja za medani hatuzipi uzito wake, ndiyo maana kwa mwaka ujao wa fedha serikali tumeongeza fedha kwenye majeshi yetu ili wajielekeze zaidi kwenda kwenye kazi zinazowahusu kuliko uzalishaji mali.

Suala la uzalishaji mali haliepukiki lakini tunapaswa kuingia ubia na sekta binafsi au kuanzisha shirika la uchumi ili kufanya kazi hii. Nalisema hili majeshi yetu yapo hapa nadhani tutaitana kuelekezana zaidi," alisisitiza.

**MSONGAMANO MAGEREZANI**

Kuhusu msongamano, Rais Samia alisema idadi ya wafungwa na mahabusu kwa sasa inalingana na alishatoa maelekezo kwa vyombo vinavyohusika kuangalia kesi ambazo ushahidi hautoshelezi na hazina mashiko ili mahabusu wapungue magerezani.

"Vinginevyo tutaweka mzigo mkubwa wa kuwalisha na kuwatunza lakini kumbe hakuna kesi za maana zinazoendelea, nitajitahidi kuongea na vyombo husika kuliangalia vizuri," alisema.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwan Kikwete (katikati), akikata utepe kuzindua maonyesho ya 23 ya kimataifa ya Build Expo, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia kwake ni Balozi wa India hapa nchini, Binaya Pradhan. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbowe, wenzake washinda kesi Sheria Vyama vya Siasa

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ) imetoa hukumu yake kuhusu kesi ya kupinga mabadiliko ya Sheria ya Vyama ya Tanzania, ikiitaka Tanzania kufanya marekebisho katika baadhi ya vipengele vya sheria hiyo kwa kuwa vinakwenda kinyume cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Kesi hiyo ilifunguliwa mahakamani huko mwaka 2019 na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na viongozi wenzake wa vyama vya upinzani.

Akisoma hukumu hiyo iliyochukua zaidi ya saa mbili jana jijini Arusha, Jaji Charles Nyachae aliyekuwa mmoja wa jopo la majaji watano waliosikiliza shauri hilo, alisema mahakama imeiamuru Tanzania kufanya marekebisho katika baadhi ya vipengele vya Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kuwa vinaenda kinyume cha Mkataba wa EAC.

Baada ya hukumu hiyo, Mbowe alisema ameridhishwa na hukumu hiyo na kuwashukuru majaji wa mahakama hiyo kwa kufanya kile alichokiita kuionyesha haki na ukweli juu ya shauri hilo.

Mbowe pia alisema hukumu hiyo imeongeza chachu ya vyama vya upinzani nchini kuendelea kufanya shughuli za siasa katika mazingira ya haki na usawa.

Alisema ana imani kubwa kwamba Serikali ya Tanzania itatekeleza maelekezo ya mahakama hiyo ya EACJ na itafanya marekebisho kwenye baadhi ya vifungu vya Sheria ya Vyama vya Siasa ambavyo vina upungufu.

"Hukumu hii ni ishara ya kutosha kuwa kweli kuna upungufu kwenye baadhi ya vifungu vya Sheria ya Vyama vya Siasa na pia ni ujumbe kwa Rais Samia," Mbowe alisema.

Alisisitiza kwamba mahakama imetimiza jukumu lake na sasa ni wajibu wa Serikali ya Tanzania kufanya marekebisho ya msingi kama ilivyoelekezwa hasa ikizingatiwa kwamba inaheshimu na kufuata matakwa kama mwanachama wa jumuiya.

"Ninaiomba serikali kupitia kwa Rais wetu, Mama Samia ione kuwa Sheria ya Vyama vya Siasa inanyooshewa vidole na majaji wa jumuiya, ni jambo la msingi na wakati umefika wa kufanyia kazi malalamiko hayo," alisema Mbowe. Kwa mujibu wa Mbowe, sasa ni wakati mwafaka kwa serikali kurekebisha sheria za nchi ili zisiwe kandamizi na kuifanya Tanzania kuwa mahali salama pa kufanya siasa zenye tija.

Wakili John Mallya aliyekuwa akiwawakilisha Mbowe na wenzake, alitaja baadhi vipengele vya Sheria ya Vyama vya Siasa, ambavyo mahakama imeelekeza kurekebishwa kuwa ni pamoja na vinavyowabana wanasiasa ambao wazazi wao siyo raia wa Tanzania kuanzisha chama cha Siasa, mahakama hiyo ikisema ni rukhsa.

Kipengele kingine ambacho mahakama imeamuru kufanyiwa marekebisho ni cha kufukuzwa mwanachama yeyote ambaye anaonekana hafai, ambapo mahakama imesema sheria hiyo ni kinyume cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa Wakili Malya, kipengele kingine ni vyama vya siasa kupeana elimu, ambapo kuliwekwa sharti kwamba ni lazima wakaguliwe na kujua ni elimu gani inatolewa.

Suala la ulinzi binafsi kwa vyama vya siasa ambalo katika sheria hiyo lilikatazwa, mahakama hiyo imesema ni rukhsa.

Kesi hiyo ya mwaka 2019 iliwasilishwa mahakamani huko na viongozi wa vyama vitatu vya siasa akiwamo Hayati Maalim Seif Sharif Hamad na Zitto Kabwe, Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo.

●**Imeandikwa na Asraji Mvungi na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

## HABARI KITAIFA

# Wanaohujumu wawekezaji kupata kibano

**Na Romana Mallya**



SERIKALI imesema imeanza kuchukua hatua ikiwamo kuwaadhibu watumishi wanaowahujumu wawekezaji wanaotaka kuwekeza Tanzania.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, (pichani) aliyasema hayo juzi jioni wakati wa mkutano wa kutia saini mkataba wa miaka mitano wa ushirikiano wa kukuza biashara kati ya Tanzania na India.

Mkataba huo kwa upande wa Tanzania ulitiwa saini na Rais wa Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), Paul Koyi na India iliwakilishwa na kiongozi wa ujumbe wa wafanyabiashara nchini humo ambaye ni Mkurugenzi wa Kanda kutoka Chemba ya Biashara India (ICC), Debmalya Banerjee.

Katika mkutano huo, yanaendelea maonyesho ya Africa Expo 2022 yaliyohusisha sekta za nishati, ujenzi na uzalishaji viwandani yanayofanyika kwa siku tatu kuanzia juzi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano huo, Kigahe alisema wizara inahakikisha inatoa msaada kwa wawekezaji katika maeneo yote ikiwa ni pamoja na kupunguza ukiritimba.

"Ukiritimba ni zaidi ya urasimu kuzungushwa zungushwa, mtu anataka kuwekeza tumesema Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kisiwahudumie wawekezaji zaidi ya siku saba. Tunapunguza urasimu ili wawekezaji wengi waje kuwekeza," alisema.

Kuhusu hatua ambazo huzichukua urasimu unapojitokeza serikalini, Naibu Waziri huyo alisema moja wamekuwa wakitoa elimu kwenye vyombo mbalimbali kwa wawekezaji ili wajue taratibu.

Alisema matatizo yaliyopo ni kwamba wawekezaji wengi kwa sababu hawajajua taratibu zinazotakiwa ili wahudumiwe wanakwenda kwa watu wasio sahihi.

"Wanakwenda kwa vishoka wale watakuzungusha, wanawazungusha wawekezaji ili wapate manufaa na kuonyesha ni vigumu kuwekeza Tanzania ili wapate nafasi ya kumpiga (mwekezaji)," alibainisha. Alisema ndiyo maana wanakitaka kituo cha uwekezaji kitoe elimu kwa wawekezaji ili waje utaratibu.

"Ukitokea ucheleweshaji huo ndani ya serikali kwa maana kituo cha uwekezaji, kweli tumeshaanza kuchukua hatua kali ikiwamo kuwapa adhabu za kinidhamu watumishi wanaoonekana wanafanya uhujumu.

"Tumeshakubaliana kwamba mwekezaji ahudumiwe ndani ya siku saba, lakini moja ya matatizo ilikuwa ni sehemu moja ya kuhudumiwa, tunataka kituo kimoja ambapo ndani yake ofisi zote zinakuwapo," alisema.

Kuhusu mkutano huo, alisema ubalozi wa India nchini unavutia wawekezaji kwa kuwaaminisha kwamba Tanzania ni sehemu salama kwa kuwekeza katika sekta za viwanda, kilimo, uchimbaji madini na biashara za huduma.

"Tumeshiriki katika maonyesho ya uwekezaji kati ya India na Tanzania hasa kwenye maeneo ya madini, ujenzi na uzalishaji katika viwanda. Tanzania tunadhamini mchango wa India kwa ushirikiano na mchango mkubwa wa uwekezaji kutoka nchi hii," alisema.

Katika hotuba hiyo mgeni rasmi ambaye alikuwa Waziri wa wizara hiyo, Dk. Ashatu Kijaji, iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Waziri, alisema takwimu za TIC zinaonyesha uwekezaji uliofanywa na India kati ya mwaka 1990 hadi Aprili 2021 ni wa Dola za Marekani bilioni 3.65 huku kampuni na taasisi 613 zikitoa ajira 48,184 kwa Watanzania.

"Kwa muda mrefu Tanzania na India kwa pamoja zinafurahia ushirikiano uliopo ambao umechangia kuwapo kwa uchumi imara na uhusiano wa kibiashara. Biashara baina ya nchi imefikia Dola za Marekani bilioni 2.22 kwa mwaka 2021/22.

"India inauza nje Dola bilioni 1.21 na kuagiza Dola bilioni 1.01. Hii inaifanya India kuwa mshirika wa tatu kwa ukubwa wa biashara baina ya Tanzania baada ya China na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE)," alibainisha.

Balozi wa India nchini Tanzania, Pradhan alisema wafanyabiashara wa Tanzania na nchi nyingine ikiwano India wamekutana siku hiyo ili kuangalia fursa za kibiashara ambazo wanaweza kuzifanya kwa ubia.

Alisema kampuni 30 kutoka India zimeshiriki maonyesho hayo na nyingine kampuni 20 zikishiriki kutoka sekta ya ujenzi.

Koyi alisema wamesaini makubaliano na India kwa sababu wanatambua nchi hiyo imepiga hatua katika teknolojia ikiwamo uongezaji wa thamani bidhaa.

"Kati ya mwezi Mei au Juni tutapeleka ujumbe wetu India, ninawaomba wanachama wa TCCIA muanze kujiandaa ili ripoti mtakapopelekewa mtumie fursa hii," alisema.

# Lori lavamia nyumba na kuua watu watatu

**Na Idda Mushi,** MIKUMI

WATU watatu wamefariki dunia na mmoja kujeruhiwa baada ya lori lililokuwa likitoka Songea mkoani Ruvuma kwenda Dar es Salaam kufeli breki na kuvamia nyumba kando kando ya barabara kuu ya Morogoro - Iringa.

Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo, Tiniheli Mdembe na Kafungili Shaaban, walisema walishuhudia dereva wa lori hilo lenye namba za usajili T 947 BQB, akiyumba na kushindwa kumudu gari katika mzunguko wa barabara ya Mikumi na kuacha njia kisha kuvamia nyumba jirani na barabara na kusababisha ajali hiyo.

"Niliona lori linakuja, likapita round about (mzunguko) mbele dereva akakutana na lori limesimama pembeni. Inaonekana alikosa breki akaamua kuhama upande wake akaingia kulia na kugonga nyumba. Miongoni mwa waliofariki dunia ni dereva wa hili lori na mtu mmoja aliyekuwa naye ndani ya gari," alisema Mdembe.

Mashuhuda hao walidai kuwa mtu mwingine aliyepoteza maisha ni msafiri anayefanya biashara ya nyanya, aliyekuwa akitokea Ruaha Mbuyuni kwenda Ifakara, ambaye wakati ameshuka kwenye gari ili avuke barabara kutafuta magari ya kwenda Ifakara na mzigo wake wa nyanya, lori hilo lililokosa mwelekeo likampamia na kumuua kabla ya kugonga nyumba.

Daktari wa zamu katika Hospitali ya Misheni ya Mtakatifu Kizito, Mikumi, Rajab Kapomba, alikiri walipokea miili ya watu wawili wanaume na majeruhi wawili, akiwemo mwanaume na mwanamke aliyekuwa akilalamikia maumivu makali ya tumbo.

"Wakati tunafanya maandalizi ya vifaa ili kumfanyia upasuaji tumbo lake liliendelea kuvimba na akafariki dunia," alisema Dk. Kapomba.

Akasema majeruhi aliyelazwa hospitalini hapo ameumia zaidi sehemu ya jicho na kwamba anaendelea na matibabu hospitalini hapo.

Jitihada zaidi kumtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna msaidizi (SACP) Fortunatus Musilim, kuzungumzia ajali hiyo, hadi jana jioni zilikuwa zinaendelea huku akipigiwa simu bila kupokea.

**"Niliona lori linakuja, likapita round about (mzunguko) mbele dereva akakutana na lori limesimama pembeni. Inaonekana alikosa breki akaamua kuhama upande wake akaingia kulia...**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **24.03.2022** mnatangaziwa hadi **05.04.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili** kuelekea **Moshi**, gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW051Z / ZG2320 KCW052Z / ZG3212 KBQ 628Z / ZE 0941**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita 28.4** |
| **Upana** | - | **Mita 5.0** |
| **Kimo** | - | **Mita 5.6** |

3. Njia itakayotumika: **Holili hadi Moshi kupitia Soweto,** gari litasafiri muda wa mchana tu ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

216769502



**NOTISI/TANGAZO**

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAIN | CHEX ENGINEERING LTD | NYUMBA YENYE HATI NA. 69065 | CHEDIEL GASPER NSHANA | BUNJU DAR ES SALAAM | 11/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ABUBAKARI ALLY WAZIRI | NYUMBA | BIG MATEI MATHIAS | MATOSA | 12/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | PRECIOUSEMMY VICTOR SHITINDI | GARI T130 DQJ HONDA SPIKE | PRECIOUSEMMY VICTOR FRANCIS | ARUSHA | 13/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | AMANI ABDUEL MSUYA | NYUMBA | AMANI ABDUEL MSUYA | BOKO CCM | 15/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | PERFECT EMMANUEL GEORGE | NYUMBA | PETER GIBSON MASSAWE | KIMARA BARUTI | 25/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | WENCESLAUS JOHN MASSAWE | NYUMBA | MATESO JOHN MASSAWE | MAVURUNZA UBUNGO | 25/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | PETER JOSSEPH ISSANGYA | GARI TOYOTA SIENTA T737 DHA | MOHAMMED ABDALLAH MOHAMMED | MAGOMENI | 14/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba ,Kiwanja au Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0713077474 / 0715363537 / 0768672367 / 0759648448 / 0628338064**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

# Uchafuzi wa Mto Mara unavyowatesa wakazi

## ● Vifo wavuvi waliohara, kutapika damu
## ● Waliokula samaki walioelea wasimulia

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

**SEHEMU ya kwanza jana ilianika picha pana ya madhara ya kuchafuliwa kwa Mto Mara na namna hali mbaya ilivyowafikia wananchi wa chini, ikiendana na hatua za kimamlaka zilizochukuliwa. Sasa fuatilia hali ya madhara kwa wakazi katika uhalisia wa maisha yao.**

KUNA usemi maarufu mitaani "mambo juu ya mambo", unaonekana kusadifu kinachoshuhudiwa kwa majirani wa Mto Mara wilayani Tarime.

Wakati madhila ya kiafya yanatua kwenye vijiji kadhaa jirani na Mto Mara wilayani hapa, nao wana upungufu wao ambao Nipashe imebaini kuwa na asilimia kubwa ya kichocheo cha madhara.

Suala la uelewa wa tahadhari za kiafya, ulinzi wa mazingira na kanuni binafsi katika kulinda afya, kwa wakazi hao bado kuna hatua nyingi nyuma, hata kufanya unapofumuka mlipuko wa madhara Mto Mara unaodumu sasa miaka minne, athari yake inakuwa ya kina kirefu kwao.

Nipashe imegundua wakazi hao wanaoishi katika nyumba za viwango vya chini na baadhi yao hawana vyoo huku mwamko wao duni kwenye kanuni za usafi wa mlo, kuanzia kunywa maji yaliyochemshwa na kutoka kwenye vyanzo salama, ni hatua mojawapo inayowakwamisha.

Ushuhuda kwenye vijiji kadhaa ni kwamba wakazi wake wamebobea kwenye maji ya Mto Mara yasiyochemshwa na imegundulika ndiyo chanzo chao pekee cha maji ya matumizi majumbani.

Gazeti hili pia limebaini hata upande wa mlo, Mto Mara uliochafuliwa, ndiyo chanzo kikuu cha mboga (samaki) inayotumiwa na wakazi wa ukanda huo ambao kwa asilimia kubwa wanajumuishwa na wafugaji, pia wavuvi.

Ni aina ya mazingira yanayotoa taswira kwa mto huo kushikilia mwenendo wa mahitaji ya maisha yao ya kila siku, huku hata shughuli mbadala za ufugaji bado nazo zinaegemea mtoni kwa mahitaji kama vyanzo vya maji kwa mifugo.

Uchunguzi huo umeibua taswira ya maisha ya kila siku katika stadi za ufugaji kwamba maji ya mtoni hayakwepeki kwa kuwa ni kawaida kwa wafugaji kuvuka maji hayo na mifugo yao kwenda upande wa pili wilaya jirani ya Butiama kusaka malisho bora.

Kingine kilichogundulika ni kwamba katika kufikia upatikanaji huduma za kiafya, upande mmoja wamekwamishwa na huduma za kiserikali kwa maana hakuna zahanati au kituo cha afya kilichoko katika mazingira yao.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Burongo, Juma Matinde anasema hadi sasa hatua iliyoko kijijini kwao Bisarwi, zahanati iko katika hatua ya ujenzi na kwa sasa wakazi wanafuata huduma umbali wa kilomita nne kijiji jirani Mtana.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), kila kijiji nchini kinapaswa kuwa na zahanati na kituo cha afya kwenye kata huku wilayani kukiwapo hospitali.

Mwenyekiti Matinde anasema kutokana na umbali ulioko wa zahanati, pia hali ngumu kuchumi, wakazi wengi wamejenga mazoea kwenda kupata huduma kutoka maduka ya dawa jirani, hata katika hatua ya juu kama madhara yatokanayo na uchafuzi wa Mto Mara, ambayo ni mabaya zaidi.

Nipashe imeshuhudia wakazi kutohofia madhara yatokanayo na maji yaliyochafuliwa, kwa kuendelea kutumia vyakula ambavyo mto huo unazalisha kama vile samaki wanaovuliwa kutoka humo.

Pia imebainika tabia ya wakazi kujipa majibu rahisi wanapokuta samaki wamekufa na kuelea, wanawala bila ya kuwa na angalizo la kiafya, hata kuchangia zaidi katika kudhurika na yaliyotokea kwa miaka minne Mto Mara.

Ndani ya mtazamo huo wa uelewa duni, Nipashe imebaini na hata kuthibitishiwa na wakazi, akiwamo Mwenyekiti wa Kitongoji Matinde, kwamba mifugo inayokufa jirani na mto imekuwa ikitupwa majini na kuchangia uchafuzi zaidi wa sumu majini. Ndiyo hali inayotawala sasa katika vijiji kadhaa vya Kata ya Manga.

**SIMULIZI YALIYOWAKUTA**

Mzee Mwita Mangati (85), ni mzazi aliyepoteza mtoto kutokana na madhara ya uchafuzi wa Mto Mara. Anasimulia mwanawe alikuwa na kikundi cha uvuvi ambacho mwaka jana waliweka kambi ya uvuvi ambayo huwa na utaratibu wa kujihudumia yote huko ikiwamo chakula.

Anasema kuwa akiwa na wenzake wawili, mtoto wake huyo aliyekuwa Mwenyekiti wa Kitongoji, alianza kujisikia vibaya huko kambini katika msimu huo ambao mto unakuwa umefurika.

Mzee Mangati anasema mwanawe na wavuvi wenzake walirejea nyumbani huku akiwa na hali isiyo nzuri kiafya, kuna siku alihudhuria mkutano wa kijiji na ghafla alianguka na kuanza kuhara na kutapika damu na umauti ukamkuta muda mfupi baadaye, akiacha watoto tisa kutoka kwa wake wawili.

Mama Nyamata Julius (45), ni mjane wa mvuvi mwingine wa kambi hiyo, anayefafanua kwamba wavuvi hao walikuwa na kawaida ya kuweka kambi kati ya siku sita na saba ambako mumewe alikutwa na madhara yatokanayo na maji yenye sumu mtoni.

Mjane huyo wa watoto watano anaeleza mumewe aliporejea nyumbani, alipata huduma katika hospitali mbalimbali, hata kupewa rufani kadhaa ndani ya Rorya na Tarime na hali yake ikawa inatengemaa na baadaye kuzidiwa kwa miezi kadhaa, katika kuhara na kutapika damu, hata akafariki dunia mwishoni mwa mwaka 2020.

Bhoke Mwita, mwenye mwonekano wa umri wa makamo, ana simulizi ya mkasa usiotofautiana sana na watangulizi wake; alipoteza mume Juni mwaka jana kutokana na kuhara na kutapika damu.

Anaeleza hali hiyo ya kutapika na kuhara ilimfikia hata yeye na wanawe ambao hakutaja idadi wala umri wao, japo madhila yao hayakuhusisha kutoa damu, Mto Mara ulipochafuka Machi mwaka huu; wote hawakufika hospitalini.

Kwa mujibu wa Bhoke, upande wa pili wa mali zao, ng'ombe sita nao walikufa kwa kuharisha damu, mama huyo akiwa miongoni mwa wanavijiji waliopoteza mifugo zaidi ya 50 kutokana na uchafuzi wa Mto Mara mwanzoni mwa mwezi huu.

Uhalisia huo wa kuteseka na uchafu kutoka Mto Mara, simulizi yake pia anayo mama anayejitambulisha kwa jina la Ghati, akieleza kuwa baada ya kula samaki wenye kasoro kiafya hivi karibuni, amekuwa akiugua na wanawe kadhaa. Anasema mumewe amenusurika kwa sababu hakuwapo.

***ITAENDELEA KESHO....**



Bhoke Mwita, mkazi wa Kijiji cha Bisarwi wilayani Tarime aliyepoteza mume Juni mwaka jana kutokana na kuhara na kutapika damu baada ya kunywa maji ya Mto Mara. **PICHA ZOTE: MPIGAPIGA WETU**



Mzee Mwita Mangati akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kijijini Bisarwi hivi karibuni.

HABARI KITAIFA

## Mradi wabadili fikra za vijana

**Na Francis Godwin,** IRINGA

BAADHI ya vijana waliokuwa wanaishi katika mazingira magumu waliokuwa na mzigo wa kutunza familia zao na hata mabinti kukimbia vijijini kwenda kufanya kazi za ndani, hivi sasa maisha yao yamekuwa tofauti baada ya kufikishiwa elimu ya ujasiriamali na ya saikolojia.

Meneja Mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), Zilipa Mgeni, aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya siku 10 kwa vijana 100 kutoka kata tatu za wilaya ya Mufindi mkoani Iringa.

Mgaya alisema kutokana na mwendelezo wa mafunzo hayo yaliyoanza mwaka jana na tathmini ndogo ambayo mradi umefanya kupitia viongozi wa vijiji na kata, wameona kuna mabadiliko makubwa.

Alisema baadhi yao wameepuka tabia za kushinda vijiweni na hata wale waliokuwa wanategemea kuendesha maisha yao kwa kwenda mijini kufanya kazi za ndani, wametulia vijijini na kufanya shughuli za maendeleo.

Kwa mujibu wa Mgeni, katika mafunzo hayo ya siku 10 yaliyoanza jana katika ukumbi wa Yatima kijiji cha Igoda, yanashirikiasha vijana ambao baadhi yao ni wale waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo mimba za utotoni.

Mgeni alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha zaidi ya vijana 770, wakiwamo watoto 150 yatima kutoka kata hizo tatu zinazohusisha vijiji 16.

Alisema mradi huo wa miaka minne ulioanza mwaka 2021, umefadhiliwa na serikali ya Finland chini ya taasisi yake ya Diaconess kwa ushirikiano wa serikali ya Tanzania chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na taasisi ya Foxes Community and Wildlife Conservation (FCWC)

Mgeni alisema baada ya mafunzo hayo kutolewa kwa walengwa watawezeshwa mitaji ya kuendeshea miradi ambayo watakuwa wamechagua kuifanya kwa kuwaongezea nguvu ya kuiboresha zaidi.

Mkufunzi wa mafunzo hayo kutoka Chuo Kikuu cha Iringa, Dk. Blandina Kivavike, alisema mafunzo hayo maalum ni ya kuwajengea uwezo katika nyanja za ujasiriamali na yatawezesha vijana hao kuondokana na fikra mgando ambazo baadhi yao wamekuwa nazo kuwa ili uwe mjasiriamali ni lazima kuwa na fedha mkononi.

"Maeneo mengi ya vijijini kuna fursa nyingi za kufanya ambazo kimsingi ni mtaji mkubwa kwa mtu ambaye anatamani kuwa mjasiriamali. Iwapo wahusika wataondokana na fikra mgando za kutegemea fedha, wanaweza kupiga hatua katika maisha," alisema.

**Mgeni alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha zaidi ya vijana 770, wakiwamo watoto 150 yatima kutoka kata hizo tatu zinazohusisha vijiji 16.**

# Balozi wa China, Dk. Mwinyi waahidi kuimarisha uhusiano

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa China nchini Tanzania, Chen Mingjian, Jumatano wiki hii alimtembelea Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi mjini Zanzibar na kufanya naye mazungumzo.

Katika mazungumzo hayo balozi Chen na Dk. Mwinyi walibadilishana mawazo kuhusu ushirikiano kati ya China na Tanzania na China na Zanzibar, taarifa kutoka Ubalozi wa China nchini ilibainisha jana.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhandisi Zena Ahmed Said, Balozi Mdogo wa China mjini Zanzibar, Zhang Zhisheng, na viongozi wengine walihudhuria mazungumzo hayo.

Pia Balozi Chen aliwasilisha salamu za kheri za Makamu wa Rais wa China, Wang Qishan kwa Rais Mwinyi huku akisema China na Tanzania, na China na Zanzibar zina urafiki wa dhati uliojengwa na Mwenyekiti Mao Zedong, Rais Julius Nyerere, Rais Abeid Karume na viongozi wengine wa vizazi vya zamani.

Alisema Uhusiano kati ya China na Zanzibar umejengwa juu ya msingi imara na umepata maendeleo makubwa katika miaka ya hivi karibuni.

Balozi huyo pia alisema China iko tayari kuchukua utekelezaji wa matokeo ya Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) kama fursa, ili kuoanisha zaidi Mpango wa Ukanda na Njia na mkakati wa maendeleo wa Zanzibar, kupanua ushirikiano baina ya nchi hizo katika miundombinu, uchumi wa bluu, kilimo na nyanja nyinginezo, na kukuza ushirikiano wa vitendo kati ya China na Zanzibar ili kuzaa matunda zaidi.

Rais Mwinyi alimwomba Balozi Chen kuwasilisha salamu zake za dhati kwa Makamu wa Rais Wang Qishan.

Dk. Mwinyi aliishukuru serikali ya China kwa msaada wake wa muda mrefu na muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar, hasa mchango wa chanjo na vifaa tiba vya UVIKO-19.

Alisisitiza kuwa Zanzibar na China siku zote zimekuwa marafiki na washirika wazuri, wakisimama bega kwa began a kwamba Zanzibar iko tayari kushirikiana na China kuendeleza kwa nguvu urafiki wa jadi uliopo na kusukuma mbele maendeleo ya uhusiano wa Tanzania na China ili kuwanufaisha zaidi watu hao wawili.

Balozi Chen pia alikutana na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla siku hiyo hiyo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Balozi wa China Tanzania Chen Mingjian, Ikulu jijini Zanzibar mapema wiki hii. **PICHA: UBALOZI WA CHINA**

# Wazazi wahadharishwa vituo malezi watoto

**Na Mary Geofrey**

KATIBU wa Chama cha Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo, amewataka wazazi na walezi nchini kupeleka watoto kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo (daycare) vilivyosajiliwa na kukidhi vigezo ili kuepuka kufanyiwa vitendo vya ukatili.

Josephine Rutashobya alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na Nipashe mkoani Dar es Salaam kuhusu uzinduzi wa chama hicho unaotarajiwa kufanyika leo.

Alisema wazazi na walezi wengi hawana uelewa wa aina ya vituo vya malezi ya watoto wao na ndiyo sababu watoto wengi wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili. "Tumeanzisha hiki chama ili wazazi wafahamu umuhimu wa vituo hivi ambavyo vinawalea watoto kwenye maadili yanayofaa wakati wazazi wanapokuwa kazini," alisema.

Katibu huyo alisema lengo la kuanzisha vituo hivyo ni kupunguza wimbi la watoto wa mitaani ambao wazazi wao wanakwenda kazini na kukosa uangalizi wa karibu.

"Wengine wameanzisha kama vitega uchumi ndio maana sasa ili kuondokana na tatizo hili, tumeona kama chama kwa kushirikiana na serikali tuhakikishe vituo vinavyoanzishwa vinakidhi vigezo," alisema.

Mwenyekiti wa chama hicho, Shukuru Mwakasege, alisema lengo mahususi la chama hicho ni kutoa elimu kwa wamiliki wa vituo vya kulelea watoto wadogo, wajue sifa zinazotakiwa kabla ya kuanzisha badala ya kuendelea kuanzisha kiholela.

"Wapo wazazi ambao wanaogopa kupeleka watoto kwenye vituo kwa sababu ya kufanyiwa vitendo vya ukatili, wawe na amani kwa sababu sasa vituo vyote vitazingatia sheria na taratibu za nchi," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kikwazo kikubwa ni serikali haijavipa kipaumbele vituo vya kulelea watoto na badala yake wanatambua kuanzia elimu ya awali.

Alisema mpango walionao wa kudhibiti matatizo hayo ni kushirikisha viongozi ngazi ya jamii, ili kusianzishwe vituo kabla ya kupitia ofisi za serikali ya mtaa.

"Mtoto chini ya miaka miwili haruhusiwi kujiunga na 'daycare' kwa sababu umri huo anatakiwa kuwa chini ya uangalizi wa mzazi au mlezi kwanza," alisema Mwakasege.

Nipashe

MWANGA WA JAMII

# Waamuzi wanaweza kumaliza hili bila VAR

**KUMEKUWA** na kelele nyingi za wadau wa soka kuhusiana na mamuzi ya waamuzi wa mpira wa miguu kwenye Ligi Kuu Tanzania bara na zile za chini.

Wadau wengi wameonesha kwamba, sasa kunahitajika teknolojia ya usaidizi wa waamuzi kwa njia ya video yaani VAR. Sababu yao kubwa ni kwamba, wanahitaji maamuzi sahihi kutoka kwa waamuzi hao ili mwenye haki ya kushinda asipokonywe.

Kama kuna kitu katika siku za karibuni kimekuwa kikiwaudhi wapenzi wa michezo ni waamuzi, hususan wa soka kutoa maamuzi yenye utata.

Ingawa tunaamini kwamba maamuzi tata yamekuwapo kwenye michezo mingi hata ya ligi za madaraja ya chini, lakini yale yanayofuatiliwa sana na kuzua mjadala ni yanayohusu klabu kubwa na zenye wapenzi wengi za Yanga, Simba na Azam.

Kuamua vibaya ni kunyima haki kwani asiyestahili ananufaika na maamuzi ya hovyo huku mwingine akiumia.

Wachambuzi wa soka wamekuwa wakionesha kwamba matukio ya waamuzi wetu kushindwa kutafsiri vyema sheria za mchezo, hususan wa soka unaopendwa zaidi nchini inavunja moyo na kuua maendeleo ya mchezo huo nchini.

Tunakubaliana na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia aliyesema hivi karibuni kwamba, maamuzi tata yamesababisha kuwapo kwa kilio kikubwa cha kutaka matumizi ya usaidizi wa waamuzi kwa njia ya video (VAR).

Ni kweli kabisa kwamba, waamuzi ni wanadamu kwa hiyo wanaweza kufanya makosa kutokana na uanadamu wao.

Lakini kama alivyosema Karia, kwa nini wanashindwa au kukataa kushirikiana katika kuona matukio yanayofanyika uwanjani kwa sababu wanakuwa zaidi ya mmoja. Kwa nini wanamwachia yule wa katikati hata kama wao wameona tofauti.

Karia alihoji kwamba kuna maamuzi mengine yanafanyika ambayo mwamuzi wa kati hakuona.

Anachokisema Karia ni kwamba, endapo waamuzi watakuwa wanashirikiana kuelezana pale mwamuzi wa katikati anaposhindwa kujua ukweli sawasawa wa kilichotokea na kuuliza wenzake kwa undani, itasaidia sana kupunguza maamuzi yanayoacha maswali na kukatisha tamaa.

Na kama alivyosema Karia, VAR ni gharama kubwa na tukiamini anachosema kwamba anakijua vyema, kupata VAR moja ni Sh bilioni 14.5 na ina kamera 33-38 za aina tofauti tofauti na kwamba hata ukiipata siyo mali yako bali inabaki kuwa mali ya aliyetengeneza.

Pamoja na serikali hivi karibuni kuonesha utayari wa kuwa na VAR, lakini kwa mtazamo wetu tunadhani kipaumbele kikubwa kwa sasa kiwe ni kuboresha viwanja kila mkoa na kushuka hadi kila wilaya kabla ya kukimbilia huko.

Tumeshuhudia mechi za ligi kuu zikichezewa katika viwanja ambavyo kwakweli hata kama vimeidhinishwa, bado vinachangia matokeo yasiyotarajiwa hasa kunaponyesha mvua.


Ni kwa mantiki hiyo tunahimiza waamuzi kujitahidi kuwa waadilifu na kutenda haki, lakini kupokea ushauri wa Karia wa kufanya ushirikiano kwenye maamuzi.

Lakini tunadhani bado mamlaka za juu zinapaswa kutoa adhabu kali zaidi kwa mwamuzi anayevurunda na hasa anaposhindwa kutafuta ushauri wa wenzake au anayeonekana dhahiri uwezo wake ni mdogo katika kutafsiri sheria 17 za soka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Utashangiliaje Stars umevaa jezi ya klabu?

**NAANZA** kwa kuipongeza timu ya soka ya Tanzania, Taifa Stars kwa ushindi wa mabao 3-1 ilioupata kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Afrika ya Kati.

Ilikuwa ni mechi ya kirafiki iliyo kwenye kalenda ya FIFA. Yalikuwa ni mabao ya Dismas Novatus, nahodha Mbwana Samata na Geogre Mpole ambayo yaliifanya Stars kutoka kifua mbele.

Kuna wanaobeza kwa kusema kuwa Stars huwa inashinda kwenye mechi za kirafiki, lakini kwenye mechi halisi za mashindano, inachemka.

Inawezekana ikawa kweli, lakini ukweli mwingine unabaki pale pale kuwa mechi kama hizi zinaisaidia Tanzania kupanda kwenye viwango vya FIFA kama timu inapata ushindi.

Labda baadhi ya mashabiki hawajui faida ya kupanda kwenye viwango vya FIFA. Ni kwamba ukiwa juu kidogo, unapata faida hata kwenye upangaji wa ratiba ya mechi za kufuzu CHAN, AFCON na hata Kombe la Dunia.

Nchi inapokuwa ipo chini, tabu inayoipata kwanza ni kuanza kwenye hatua za awali, huku zile za juu zikisubiri raundi ya kwanza.

Kuna nchi ni aghalabu sana kuona zikicheza mechi ya mtoano. Pili ni kwamba ukiwa chini sana unapangwa na timu kongwe, ngumu na zoefu kwenye michuano mbalimbali ya Afrika, hivyo inakuwa ngumu 'kutoboa'.

Angalau usogeesogee unaweza kupata kigogo mmoja, lakini kama kwenye viwango vya FIFA uko chini, unaweza kujikuta umewekwa na vigogo wawili na hapo ndipo inapokuwa mtihani.

Utamaduni na soka kote duniani ni kwamba timu zenye viwango vya juu, zinakuwa kwenye kapu moja, hivyo ni nadra sana kukuta zikiwa kwenye kundi moja.

Lakini zile za chini ndizo zinapata tabu sana kwa sababu zinatafutiwa vigogo vya kuwekwa nao kundi moja, hivyo kusaka ushindi kwenye mechi kama hizi ili kupanda viwango japo taratibu taratibu ni jambo la msingi sana na linaweza kuwa na faida kubwa hapo baadaye.

Kwenye mechi dhidi ya Afrika ya Kati nimeona tabia ambazo zimeanza kuota mizizi kwa baadhi ya mashabiki kuvaa jezi za klabu zao badala ya timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Hii haipendezi na si uzalendo kabisa, kwani timu ya taifa ndiyo inaanza na klabu zinakuja baadaye.

Nimeshuhudia baadhi ya mashabiki wa Simba wamevaa jezi za klabu yao, halafu eti wanaishangilia timu ya taifa. Huo ni utovu wa nidhamu. Wale wa Yanga nao wamevaa jezi za klabu yao, lakini wanaishangilia Stars. Si uzalendo hata kidogo.

Sasa kuna wengine walionekana kuvaa jezi za Liverpool, Manchester United, Chelsea, lakini wapo Uwanja wa Benjamin Mkapa wakiishangilia Stars. Hii haikubaliki.

Sitaki kusema kuwa eti walinzi wa mlangoni wawazuie mashabiki waliovaa jezi za timu zingine wasiingie uwanjani, lakini nataka kuwashauri mashabiki waanze utamaduni wa kuvaa jezi ya timu ya taifa, kama Stars inacheza.

Kuishangilia Stars huku umevaa jezi za timu nyingine ni sawa tu na unafiki. Hii ni timu ya Watanzania, inabidi watu wawe wa Utaifa, mengine baadaye. Ikicheza Simba, Yanga wanavaa jezi ya klabu, lakini kwa nini ikicheza Stars wanashindwa kuvaa jezi ya timu ya taifa.

Nchi nyingine huwezi kuona hilo, kwa sababu watu wanajivunia mno nchi yao. Niliangalia mashabiki wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo wakati ikijiandaa kucheza na Morocco jana jinsi walivyovaa, na ushangiliaji wao, ni hatari tupu na huwezi kujua nani ni shabiki wa timu gani.

Hivi kama shabiki unaweza kununua jezi ya klabu yako, unashindwa kununua ya Taifa Stars? Kama huwezi kweli una uzalendo? Timu hii pia ina wadhamini wake, na jezi zake zinauzwa na mashabiki wanatakiwa wanunue ili kuichangia timu, lakini pia kuitangaza kampuni ambayo inaidhamini, badala yake mashabiki waendelea kuzitangaza zile ambazo hazihusiki na timu hiyo ya taifa.

Nadhani imefika wakati Watanzania kuipenda Stars kama wanavyozipenda timu zao za hapa nchini na nje ya nchi na si kuipenda kinafiki, ili watu wasiwafikirie vibaya.

Halafu si lazima, mtu hataki kununua jezi, au haoni umuhimu huo, basi aje tu uwanjani akiwa amevaa kiraia tu, wala haikatazwi. Tununue jezi za Stars na kuzivaa inapocheza. Sivyo nenda na nguo za kawaida tu.

Lakini kuvaa jezi za klabu nyingine kwenye mechi ambayo inacheza Taifa Stars, kunashangaza, kusikitisha na kufikirisha kwa wakati mmoja.

## Wahitimu kidato cha 6 wapewa neno

Na Mwandishi Wetu,
SENGEREMA

WAHITIMU wa kidato cha sita wametakiwa kusoma kwa bidii ili kupata ujuzi utakaowawezesha kusukuma kwa kasi maendeleo ya nchi kwenye fani mbalimbali.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bahati Geuzye, alipokuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya 33 ya kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Sengerema mkoani Mwanza.

Katika mahafali hayo, wanafunzi 576 kutoka tahasusi 10 za sayansi, biashara na sanaa wanatarajia kuhitimu masomo hayo Mei, mwaka huu.

"Mnapaswa kujiandaa vya kutosha kwa sababu taifa linawategemea mje kulitumikia kwenye fani mbalimbali, hivyo hakikisheni mnafaulu kwa viwango vya juu mpate taaluma zitakazosaidia kusukuma maendeleo ya nchi yenu," alisema.

Geuzye alisema ili taifa lisonge mbele kwa kasi kiuchumi, linapaswa kuwa na wasomi waliobobea kwenye taaluma mbalimbali badala ya kutegemea wataalamu kutoka mataifa mengine.

Aliwataka wanafunzi hao kujifunza uzalendo na uaminifu kwa nchi yao ili watakapopata kazi mara baada ya kumaliza shule waiwezeshe nchi kupiga hatua kubwa kimaendeleo kwa kasi.

Mkurugenzi huyo alipongeza uongozi wa shule na wanafunzi wa shule hiyo kwani takwimu zinaonyesha kuwa imekuwa ikifanya vizuri kitaaluma mwaka hadi mwaka na aliwataka wasibweteke na mafanikio hayo.

"Mmekuwa mkifanya vizuri nawaomba muendelee kufanya vizuri zaidi na ikiwezekana muwe kwenye 10 bora kitaifa mwaka huu na naamini mkiweka nia mtafanikiwa kufika kwenye kumi bora," alisema.

Shule ya Sekondari Sengerema yenye wanafunzi 1,306 ni miongoni mwa shule 17 kongwe za sekondari ambazo zilikarabatiwa kwa uratibu wa TEA na imeshatumia Sh bilioni moja kukarabati shule hiyo mwaka 2017/2018.

# Waliokataa kuondoka hifadhi Saadani kufanyiwa tathmini

Na Munir Shemweta,
BAGAMOYO

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesema kaya 18 zilizokataa kuondoka kitongoji cha Uvinze ndani ya Hifadhi ya Saadan, Bagamoyo mkoani Pwani, zitafanyiwa tathmini na timu ya wataalamu wa kisekta, mkoa na wilaya.

Hatua hiyo inatokana na kaya hizo kugoma kuondoka eneo la hifadhi ya Saadan kwa madai kwamba hapo ni asili yao na njia yoyote ya kulazimishwa kuondoka inawafanya kupoteza asili yao ambayo baba na babu zao waliishi hapo.

Tayari baadhi ya kaya zimeondoka eneo hilo la Hifadhi ya Taifa ya Saadan baada ya kufanyiwa uthamini na kulipwa fidia.

Timu ya mawaziri wa wizara za kisekta ikiongozwa na mwenyekiti wake, Dk. Mabula iliruka kwa helikopta kujionea kaya zilizoko ndani ya hifadhi hiyo ikiwa ni njia ya kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

Mawaziri walioko kwenye ziara hiyo itakayowafikisha pia mikoa ya Morogoro, Arusha, Mara, Kigoma na Mbeya mbali na Dk. Mabula ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega; Mary Masanja ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na Hamis Chilllo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Pia wamo makatibu wakuu wa wizara za kisekta na wataalamu kutoka wizara hizo.

Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Saadan, kitongoji cha Uvinje, ambacho kaya 18 zimo ndani ya hifadhi juzi, Dk. Mabula alisema wataalamu wa kisekta, mkoa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo watapita kufanya tathmini wa kina katika kijiji hicho.

"Taratibu zote zitafanyika. Tukiondoka hapa tutaacha wataalamu watafanya tathmini na kama mtabaki au mkiondoka mtaambiwa na lolote litakaloamuliwa baada ya tathmini, tunaomba ushirikiano wenu na hakuna sehemu serikali inatumia mabavu," alisema.

Baadhi ya wakazi wa kaya hizo, waliuelezea ujumbe wa mawaziri hao kuwa uamuzi wa kuhamishwa eneo wanaloishi hauzingatii misingi ya haki kwa kuwa wameishi eneo hilo kwa muda mrefu tangu mababu na baba zao.


Walisema wananchi wa kijiji hicho wamekuwa wakitambulika na kushiriki shughuli zote zikiwamo za uchaguzi kwa muda mrefu, hivyo wanashangazwa na suala la kutakiwa kuondoka.

"Uamuzi wa kutuhamisha hapa lazima uende sambamba na sababu za wao kuhama na kuelezwa pia umbali wa kitongoji chao na hifadhi ya Taifa ya Saadan kwa lengo la kuelewa uingiaji wao kwenye hifadhi," alisema Rajabu Abdallah.

Naye Naibu Waziri Masanja aliwataka wananchi hao kuelewa kuwa sheria ya Tanzania inaeleza wazi kuwa umiliki wa ardhi si wa mtu yeyote na unapohitajika wakati wowote na serikali, unachukuliwa lakini kinachoangaliwa ni haki za binadamu.

Ulega kwa upande wake aliwaeleza wananchi hao kuwa suala la wananchi kuhama eneo moja kwenda lingine ni la kawaida kwa kuwa hata Mtume Muhammad pamoja na kuzaliwa mji mtakatifu wa Maka, alihamia Madina na kuacha kila kitu na kuwataka wakazi hao kutafakari msimamo wao kwa kuzingatia pia masuala ya imani ya dini.

Timu ya mawaziri wa wizara za kisekta iko katika ziara ya kutembelea maeneo yenye migogoro ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya kupeleka mrejesho wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bima ya Alliance, Krinshnan Anantha (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa uzinduzi wa ushirikiano wa makampuni ya Airtel na Axeiva, ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za bima kidigitali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waonya kupandisha bei sukari Ramadhani

Na Mary Geofrey

KUELEKEA mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Kampuni ya Sukari Kilombero imewatoa hofu wananchi kuwa haitapandisha gharama ya sukari.

Vilevile, imewataka wafanyabiashara nchini kutopandisha bei ya sukari kutokana na historia ya kupandishwa kwa bidhaa za vyakula katika msimu huo.

Mkuu wa Idara ya Biashara kutoka Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Fimbo Butallah, alibainisha hayo juzi mkoani Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema kiwanda kina akiba ya sukari tani 20,000, hivyo hakuna sababu ya kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo.

"Lengo la mkutano wetu sisi Kilombero kupitia chapa ya 'Bwana Sukari' ni kuwatoa hofu Watanzania hasa tunapoelekea kwenye mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwamba bei ya sukari haijapanda na hatutarajii ipande," alisema.

Fimbo aliwataka wafanyabiashara wote wa jumla na rejareja kutokujaribu kupandisha bei ya sukari ili kuepuka kile ambacho kimekuwa kikijitokeza wakati wa mfungo huo miaka iliyopita.

"Muda kama huu ukifika bei za vyakula vingi vinapanda, watu wanachukua kama fursa ya kupata faida isiyokuwa na sababu yoyote lakini sisi tunawaonya bei ya sukari, sisi kama wazalishaji hatujapandisha, hakuna muuzaji wa Bwana Sukari atakuwa na sababu yoyote ya kupandisha bei," alionya.

Aliongeza: "Tunaomba watu wote wafurahie mfungo huu wakiwa wanapata sukari ya kutosha kwa sababu sisi tunayo sukari ya kutosha katika maghala yetu ambayo yatatuvusha salama katika mfungo huo, hakuna sababu ya kuleta taharuki kwa wananchi wala kwa wanaofunga," alisema.

Mkuu wa Idara huyo alisema tayari wameshaanza mchakato wa kuingiza sukari zaidi kutoka nje ya nchi, akibainisha kuwa itaanza kuingia nchini muda wowote kuanzia sasa kwa kuwa wamepewa kibali ya kuagiza tani 5,000.

"Tumeshaanza utaratibu wa kuagiza sukari itaanza kuingia nchini muda wowote kuanzia sasa," alisisitiza.

Alisema mwakani wataongeza kiwango cha uzalishaji wa sukari kutoka tani 130,000 hadi tani 270,000 kwa mwaka baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda chao kilichoko mkoani Morogoro.

"Kiwanda kitakamilika mwaka 2023 na tutaanza kutoa sukari ya kutosha na itasaidia kwa kiasi ki-



Makandarasi kutoka mikoa mbalimbali wakimsikiliza Wakili wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Salehe Njaa (mbele), wakati akitoa mada kuhusu umuhimu wa kufanyakazi kwa ubia, katika mafunzo kwa makandarasi hao yanayoendelea mkoani Dodoma juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Makandarasi wahadharishwa miradi ya ubia

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB), imewataka makandarasi kuwa makini wanapotaka kufanya miradi ya ubia ili kuepuka migogoro ambayo inaweza kusababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana mkoani hapa na Mwanasheria wa CRB, Salehe Njaa, wakati akitoa mada kuhusu muundo mzuri wa utekelezaji wa miradi ya ubia kwenye mafunzo kwa makandarasi yanayoendelea jijini hapa.

Alisema miradi ya ubia ni kama ndoa ambayo iwapo mhusika atashindwa kuchagua mtu makini wa kuwa naye ataishi kwa shida, hivyo ni vyema wakachukua muda kuangalia aina ya watu wa kuwa nao kwenye ubia huo.

Njaa alisema wateja wengi kwa sasa wanapenda makandarasi wanaofanya kazi kwa ubia, hivyo akawashauri makandrasi hao nao kufanya miradi ya ubia kwa kuwa kuna faida nyingi isipokuwa wawe makini na watakaoingia nao ubia.

"Lazima ujiulize watu unaotaka kuingia nao mkataba kwenye mradi wa ubia kama wanauwezo wa kimtaji, wanajituma na ni waaminifu kiasi gani kwa sababu ukiingia kichwa kichwa unaweza kujikuta pabaya.

"Mchunguze huyo mtu ana miradi wapi na aliikamilishaje, kwa sababu unaweza kukuta ana miradi miwili sehemu na yote haijakamilika kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa hivyo jipe muda wa kutosha usiharakishe," alisema

Pia alisema ni muhimu watu wanaotaka kufanya miradi ya ubia kufahamu miiko ya kazi ya ukandarasi kwani uzoefu unaonyesha kwamba baadhi wamekuwa wakitumia fedha za miradi kufanya shughuli zingine hivyo kukwamisha miradi iliyolengwa.

Alisema kuna baadhi ya makandarasi ambao wanaamini katika njia za mkato na hawafuati miongozo ya kazi za ukandarasi hali ambayo inaweza kuleta shida wakati wa ufanyaji kazi.

"Kuna mtu ana kampuni ya ukandarasi lakini haamini kwamba kuna ulazima wa kuwa na mhasibu wala mtu wa manunuzi, anafanya mambo kiholela holela tu sasa ukiwa naye huyu lazima mtasumbuana huko mbele ya safari," alisema.

Njaa aliwataka makandarasi hao pia kuangalia uwezo wa watu wanaotaka kuingia nao ubia kama wana uwezo wa kifedha angalau kidogo ili waweze kuchangia mtaji wa kuanzia pale wanapopata kazi za ujenzi.

"Hapa sisemi kwamba lazima awe na fedha nyingi sana, maana unaweza kuingia ubia na mtu hata mnapopata kazi ukimwambia achangie milioni mbili tu hana sasa hapo utakuwa umeingia ubia wa nini," alisema.

Wakili Njaa alisema kitu kingine cha muhimu cha kuzingatia ni uwajibikaji wa watu wanaoingia nao ubia kwani baadhi ya makandarasi wakishaingia ubia wamekuwa wakiwategea wenzao na hawaendi kwenye usimamizi wa miradi husika.

Alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha migogoro baina yao na wengi wamekuwa wakishitakiana kwa CRB na wakati mwingine kutaka kuvunja makubaliano waliyoingia.

"Kuna watu watatu waliingia kwenye mradi wa ubia sasa wawili wakaandika barua kwa bodi kwamba wanataka kumwondoa sisi tukamwita na kumhoji tukagundua kwamba hawajibiki kwenye ubia huo na hajaonekana site (kwenye eneo la mradi) kwa miezi mitatu anategea wenzake," alisema.

Alisema makandarasi wanaotaka kuingia kwenye kazi za ubia wanapaswa kuchagua watu wawazi na wanaoaminiana hasa kwenye masuala ya fedha ili kuacha tabia ya kufuatana kila sehemu wanapokwenda kufanya manunuzi.

Wakili Njaa alisema kuna mteja alikuwa akifanyiwa kazi yake na makandarasi walioingia ubia kwenye mradi wake na ilitokea kwa muda mrefu hawakuonekana eneo la mradi na ndipo akaamua kushtaki kwa bodi ya makandarasi.

"Sisi tuliwapigia simu wote kuwauliza kulikoni mbona mteja anawalalamikia mko wapi? Cha kushangaza wote wakatuambiwa kwamba wako China, tulipowauliza wote wameenda kufanya nini wakasema wameenda kufanya manunuzi ya vifaa vya ujenzi. Kumbe tatizo hapo hawaaminiani kwa sababu kama wangeaminiana angeenda mmoja tu," alisema

# Waziri ataka ulinzi wa ardhi kuepuka migogoro isiyo tija

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezitaka taasisi na watu binafsi kuhakikisha wanalinda maeneo yao na kuweka mipaka kuepusha uvamizi na migogoro isiyoisha.

Mabula aliyasema hayo jana kwenye kikao cha kujadili masuala ya migogoro ya ardhi kilichohusisha mawaziri kutoka katika wizara za kisekta za ardhi, utalii, mifugo na uvuvi na mazingira walipokutana Pwani na kutembelea kwenye maeneo yenye migogoro.

Alisema kila taasisi ina wajibu wa kulinda maeneo yao hasa baada ya kupata hati miliki ili kusiwepo na migogoro.

"Na haya ni maelekezo kwa nchi nzima. Taasisi au mtu binafsi aliyemilikishwa ardhi ni jukumu lake kulinda ardhi. Siyo mtu anakaa miaka sita haendelezi ardhi halafu anategemea wizara ya ardhi imlindie," alisema Mabula.

Pia alisema maeneo yote ambayo yana hati ya serikali ni lazima yarudi kwenye mikono ya serikali kwa kuwa wizara inahitaji kukomesha tabia ya uvamizi kwenye maeneo yenye hati miliki.

"Maeneo ya serikali yasiguswe na wizara haitakuwa tayari kuwalinda wavamizi. Tukiendelea kuulea uovu mwisho wa siku serikali itashindwa kufanya kazi nyingine na katika hilo basi ni kutokuruhusu uvamizi uendelee," alisema.

Waziri Mabula alisema ziara hiyo inayohusisha wizara za kisekta inaanza awamu ya pili ya kuzungukia maeneo yenye migogoro ya ardhi katika mikoa mingine baada ya kumaliza awamu ya kwanza kwenye mikoa saba.

Kwa mujibu wa waziri huyo serikali imefuta hifadhi ya msitu ulioko Mkuranga ambao una ukubwa wa zaidi ya ekari 454 na kutoa maagizo eneo hilo ligawiwe kwa wananchi.

Mabula alisema kwa kuwa serikali imetoa maelekezo hayo, haimaanishi wananchi waanze kujigawia badala yake wanatakiwa kusubiri utaratibu kutoka mamlaka husika.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliwaeleza mawaziri hao kuwa mkoa huo ni wa uwekezaji, lakini kikwazo kilichoko kwa sasa ni baadhi ya watu kutoheshimu sheria.

Kunenge alisema udhaifu na uzembe kwa wenye hatimiliki za ardhi katika mkoa huo kishindwa kulinda maeneo yao inasababisha migogoro kuendelea.

Hali hiyo, alisema imesababisha kuchelewesha maendeleo kwenye baadhi ya maeneo na badala yake kujikita kushughulikia migogoro.

## Watumia kamera kufuatilia wanyama waharibifu

**Na Salome Kitomari,** BABATI

HIFADHI ya Jamii ya Burunge (WMA), Tarafa ya Mbugwe, Wilaya ya Babati Vijijini, mkoani Manyara, imeanza kuweka kamera za kufuatilia mienendo ya wanyamapori na kuwafukuza kabla hawajasababisha uharibifu kwenye mashamba na makazi ya wananchi.

Mradi huo utaanza kwa mfano katika Kijiji cha Sangaiwe, ikiwa ni moja ya vijiji 10 vilivyotoa eneo lenye ukubwa kilomita za mraba 283 ambazo ni za WMA inayotumika kwa shughuli za utalii na kuwawezesha kupata mapato.

Akizungumza jana na wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), wanaotekeleza mradi wa Tuhifadhi Maliasili wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Mwenyekiti wa WMA, Hamis Ngimba, alisema mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, Arusha.

Alisema lengo la mradi huo ni kutatua migogoro baina ya wanyamapori na binadamu kwa kuwa na kamera kwenye njia zao ambazo zitatuma taarifa kwenye simu za askari ambao watakwenda kuwarudisha hifadhini.

"Tumefurahi sana uwapo wa mradi huu ambao tunahamasisha wananchi waupokee hasa kijiji cha Sangaiwe ambao kimepakana na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na kinaeneo la WMA, tunaamini utasaidia sana kufukuza wanyama kabla hawajasababisha madhara," alisema.

Alisema mradi ni wa miaka mitano na zitasambazwa kwenye vijiji vyote na baadaye yatatolewa magari ya kuwezesha kufukuza wanyama hao.

Nao, baadhi ya wananchi wa kijiji cha Sangaiwe, walisema mradi huo utawasaidia kupunguza changamoto kwa kuwa wanyama wanakula mazao, kuua watu na kujeruhi na kwamba kwa msimu huu hawatarajii mavuno yoyote kutokana na uharibifu.

"Manufaa ya utalii ni makubwa kwenye kijiji chetu tumejenga shule, zahanati ya kisasa, tuna ofisi nzuri ya kijiji, imefika wakati hakuna kuchangishana na tusaidie ada kwa watoto wa kijiji chetu wanaofaulu kwenda chuo kikuu," alisema Stella Mompome na kuongeza;

"Changamoto za kuishi na wanyama ni kubwa ila tunaangalia faida maana tunapata fedha, ujio wa mradi wa kuweka kamera utaleta mafanikio makubwa maana sasa tutajua wanyama wako wapi na askari wetu watakwenda kuwafukuza tofauti na awali wananchi wakifika shamba wanakuta mazao yameshaliwa."

Awali, Katibu wa Burunge WMA, Benson Mwaise, alisema migogoro baina ya wanyama na binadamu inaongezeka kutokana na kuongezeka kwa watu ambao wanatumia maeneo ya vijiji ambayo zamani yalikuwa mapori yakitumiwa na wanyama.

Alisema licha ya changamoto hiyo wanawaelimisha wananchi umuhimu wa uhifadhi na faida zilizoko, kwa kuwa wamejenga huduma za kijamii kwa fedha hizo bila kuchangishana na lazima wajifunze kuishi na wanyama kwa kuwa wote wanahitajiana.





## Dodoma yatekeleza miradi ya bilioni 86/-

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, imetekeleza miradi ya kimkakati yenye thamani ya Sh. bilioni 86.7.

Mchumi wa Jiji, Fransic Kaunda, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya miradi iliyotekelezwa ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wa Rais kwa viongozi wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT).

Kaunda alitaja miradi hiyo ni pamoja na ile ya fedha za UVIKO-19 zilizojenga madarasa na kitega uchumi cha hoteli yenye gharama ya Sh.bilioni 59.3 katika eneo la mji wa kiserikali Mtumba.

Alisema miradi mingine iliyotekelezwa kwenye kipindi hicho ni hoteli ya Dodoma City unaojengwa kwa thamani ya Sh.bilion 1.9 kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji.

"Katika mradi huu wa hoteli ya Dodoma City imetwaa pia eneo la ziada katika kuhakikisha inakuwa na eneo la kutosha ambalo limegharimu Sh. bilioni 1.9 ambalo hadi sasa milioni 946.3 zimeshalipwa kwa ajili ya fidia kwa waliokuwepo,"alisema

Alisema hadi kukamilika kwa hoteli hiyo, Halmashauri ya Jiji inatarajia kuingizia jumla ya Sh.milioni 800 kwa mwaka kutokana na mapato ya kodi.

Mchumi huyo alisema ndani ya mwaka mmoja huo pia halmashauri imetekeleza mradi wa ujenzi wa soko la wazi la machinga lenye thamani ya Sh.bilioni 7.5 ambapo hadi kukamilika kwake litaingiza mapato halmashauri hiyo Sh. bilioni 1.1 kwa mwaka.

"Ushuru huo utakaokusanywa kwenye eneo hili ni pamoja na maegesho ya magari,vyoo vya kujisaidia,mbao za matangazo na huduma za mashine za kutolea pesa , kuchoma nyama na baa," alisema.

Katibu Mkuu wa ALAT, Elirehema Kaaya, akizungumza baada ya ziara hiyo alipongeza halmashauri kwa kutenga maeneo na kujenga vitega uchumi vitakayowaingizia mapato makubwa ya fedha.

# Tril. 4.3/- UN kuleta neema Tanzania

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetia saini makubaliano ya programu mpya ya miaka mitano (2022-2027) ya ushirikiano na mashirika yaliyo chini ya umoja wa mataifa (UN) itakayogharimu Sh. trilioni 4.3 katika kuleta afua ya mambo mbalimbali.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kutia saini makubaliano hayo.

"Leo tulikuwa na majadiliano na taasisi zinazofanya kazi chini ya UN na tumetiliana saini makubaliano kuendeleza ushirikano na nchi yetu kwa kutia saini programu mpya ya ushirikiano ya miaka mitano ambayo itaanza rasmi Julai 1, mwaka huu," alisema.

Pia alisema katika kipindi hicho cha miaka mitano, maeneo yatakayofanyiwa kazi ni elimu, afya, maji, usawa wa kijinsia, kilimo, kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini.

"Shughuli zote zitasimamiwa na wizara za kiutendaji na sisi Wizara ya Fedha na Mipango tutabaki kama wasimamizi wa shughuli zote" alisema Tutuba.

Kadhalika, alisema kwa mujibu wa UN, kiasi cha fedha hizo kitakuwa kinabadilika kila mwaka kulingana na wadau wengine watakavyokuwa wanajitokeza kusaidia katika kutekeleza miradi itakayoleta afua kwa jamii mbalimbali nchini.

"Tutaomba programu hii kabla ya Rais Samia Suluhu Hassan kuizindua rasmi. Kama hatakuwa yeye basi kiongozi yeyote mkubwa aje afanye uzinduzi, " alisisitiza Tutuba.

Pia alisema katika kipindi hicho cha miaka mitano, watatekeleza miradi kwa kuzingatia vipaumbele ambavyo vitasaidai kulinda mafanikio ya kiuchumi yaliyopatikana.

Aliishukuru UN kwa msaada ambao imeendelea kulipatia taifa katika kuleta afua za masuala mbalimbali yakiwamo afya, elimu, kilimo na usawa wa kijinsia.

Tutuba alisema kwa kushirikana na wadau mbalimbali wa UN, Tanzania imepata mafanikio mbalimbali ikiwamo kufikia uchumi wa kati mwaka 2020 kwa ukuaji endelevu wa asilimia 6.7.

"Mafanikio mengine ni kupunguza umaskini kutoka asilimi 38.4 mwaka 2007 hadi asilimia 26.4 mwaka 2018 na umri wa kuishi nchini umeongezeka kutoka miaka 50.8 hadi miaka 65.5 mwaka 2018 pamoja na ongezeko la kuandikisha wanafunzi wa elimu ya msingi," alisema.

Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Zlatan Milisic, alisema watahakikisha wanafanikisha makubalianao yote waliyofikia na serikali katika mpango huo wa miaka mitano ili kuendelea kuleta afua katika nyanja mbalimbali.



Meneja Uendeshaji wa PanAfrican Energy Tanzania (PAET), Peter Sololo (kulia) na Meneja Miradi wa Kampuni ya China Petroleum Technology & Development (CPTDC), Gao Jinwei, wakibadilishana hati za kukamilisha makabidhiano ya ufungaji wa mfumo wa mgandamizo wa gesi, unaotarajiwa kuongeza uzalishaji wa gesi wa PAET kwa asilimia 30, katika kituo cha uzalishaji wa gesi kisiwa cha Songo Songo wilayani Kilwa mkoani Lindi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafungwa miezi sita udanganyifu wa kazi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Dodoma imewahukumu kifungo cha nje cha miezi sita, Mabula Kanga na Joel Kimatare, kwa kufanya udanganyifu kwenye usaili wa nafasi za uhandisi ujenzi uliokuwa ukiratibiwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Denis Mpelembwa, baada ya kujiridhisha na maelezo ya mashahidi na vielelezo vilivyowasilishwa mahakamani.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Meshack Lyabonga, alidai kuwa tukio hilo lilitokea Mei 08, 2021 katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) baada ya sekretarieti hiyo kumkamata Kimatare, aliyefika eneo la usaili kwa ajili ya kumfanyia usaili Kanga.

Alidai kuwa Kanga aliitwa kufanya usaili huo kwa ajili ya taasisi ya Watumishi Housing Company na badala yake akamtuma Kimatare kumfanyia usaili huo huku akitambua ni kosa kisheria.

"Kimatare alipofika kufanya usaili, alikaguliwa vyeti na kuruhusiwa kuingia ndani ya chumba cha usaili na kuandika na kwa makusudi alikwenda kukaa pasipo kujisajili kwenye orodha ya wasailiwa akihofia kukamatwa.

"Baada ya usaili, maofisa wa Sekretarieti ya Ajira walihakiki idadi ya wasailiwa waliojisajili kabla ya usaili na idadi ya wasailiwa baada ya usaili na kubaini uwapo wa msailiwa mmoja ambaye hakuwa amejisajili.

"Maofisa hao walimtaka msailiwa ambaye hakuwa amejiandikisha asimame ili ahudumiwe na ndipo Kimatare alisimama na kujitambulisha kwa jina

la Kanga na alipotakiwa kutoa vyeti vyake na kitambulisho, ikabainika kuwa yeye anaitwa Joel Kimatare na si Mabula Kanga," alidai.

Baada ya kukamatwa, mtuhumiwa Kimatare alichukuliwa na Jeshi la Polisi na kufunguliwa kesi kwenye mahakama hiyo.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa watuhumiwa ili iwe fundisho kwa wengine kwa kuwa vitendo hivyo vinatia aibu kwa vijana wasomi katika jamii.

Akitoa ushahidi wake, Naibu Katibu anayesimamia masuala ya TEHAMA na ambaye kwa sasa ni Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira

katika Utumishi wa Umma, Mhandisi Samwel Tanguye, alieleza mahakama kuwa yeye ni Msimamizi wa Mfumo wa Ajira Portal ambao umemtambua

Mabula Kanga kuwa ndiye aliyeomba kazi za uhandisi na namba ya usaili ilitumwa kwenye akaunti yake.

"Ni dhahiri kuwa wawili hawa waliwasiliana ili kupeana namba za usaili ambazo Joel Kimatare alizitumia wakati wa usaili wa kuandika," alidai.

Naye Ofisa Utumishi wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Ally Mnyimwa alidai kuwa alimruhusu Kimatare kuingia ndani ya chumba cha usaili baada ya kumkagua vyeti mlangoni kabla ya kuwakwepa maofisa waliokuwa wakikagua vitambulisho.

Washtakiwa hao walikiri kufanya makosa hayo na kuiomba mahakama iwasamehe kwa kuwa ilikuwa ni mara yao ya kwanza kufanya kosa hilo.

Kanga aliiomba mahakama imhurumie kwa kuwa ana watoto wanne wanamtegemea huku Mabula akiiomba mahakama imhurumie kwa kuwa alikuwa akimuuguza mama yake mzazi.

Baada ya ushahidi na utetezi huo, Hakimu Mpelembwa aliwahukumu kifungo cha nje miezi sita na kuwataka kutokufanya makosa ndani ya kipindi hicho tangu kutolewa kwa hukumu hiyo.







Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui (wapili kulia), akikabidhi mafuta ya kula kwa Mkuu wa Kitengo cha Wazazi cha Hospitali ya Mnazi Mmoja, Magret Selvesta Tayari, msaada uliotolewa na Taasisi ya Ahmad Mohamed Al-falasi, jijini Zanzibar jana, kwa ajili ya watumishi wa wizara hiyo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kifua kikuu chaongoza kusababisha vifo duniani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KABLA ya kuibuka kwa janga la UVIKO-19 duniani, ugonjwa wa kifua kikuu ulikuwa unaoongoza kwa kusababisha vifo kati ya maradhi yanayoambukiza, taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO), inaonyesha kwamba janga la corona limesababisha kuongezeka kwa vifo kwa watu wanaougua kifua kikuu.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa Afya Hassan Khamis Hafidh, wakati akizungumza na waandishi wa habari wizarani kwake Mnazimmoja mjini hapo kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani ambayo huadhimishwa Machi 24, kila mwaka.

Alisema kwa mujibu wa ripoti ya WHO ya mwaka 2021, kifua kikuu ni kati ya magonjwa 10 yanaoongoza kwa vifo ulimwenguni.

Alisema takwimu za mwaka 2020 zinaonyesha watu milioni 10 waliugua kifua kikuu duniani, watu milioni 1.5 walikufa, sawa na wastani wa vifo 4,100 kwa kila siku.

Alisema kwa upande wa Zanzibar, mwaka 2021 jumla ya wagonjwa 1,090 waligundulika na maradhi hayo ikilinganishwa na wagonjwa 1,074 waliogunduliwa mwaka 2020.

"Ijapokuwa idadi hii inaonekana ni kubwa, lakini bado ipo chini ya makadirio ya wastani wa wagonjwa 1,600 wanaokadiriwa kuugua maradhi hayo kila mwaka hapa Zanzibar," alisema.

Vile vile, alisema bado jamiii ina uelewa mdogo ya dalili za ugonjwa huo na kuchelewa kufika katika vituo vya afya ikiwa ni miongoni mwa sababu zinazochangia kutofikia idadi ya wagonjwa waliokadiriwa kugundulika kila mwaka.

Alisema, kaulimbiu ya mwaka huu katika maadhimisho hayo "Wekeza kumaliza kifua kikuu, okoa maisha" ambayo inasisitiza haja ya dharura ya kuwekeza zaidi rasilimali na nyenzo nyingine ili kukabili mapambano dhidi ya kifua kikuu na kufikia lengo la kutokomeza ugonjwa huo.

Kaulimbiu ya mwaka huu inatoa tahadhari kwamba viwango vya fedha za kukabiliana na kifua kikuu mwaka baada ya mwaka bado ni vidogo na bila ya kuwa na rasilimali za kutosha za kifedha vita hivi dhidi ya ugonjwa huu hasa katika kukabiliana na athari zinazotokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 havitafanikiwa.

Alisema Serikali ya Zanzibar imefanya juhudi za kutokomeza maradhi hayo, ikiwa ni pamoja na kununua mashine za kisasa zenye uwezo mkubwa wa kugundua vimelea vya kifua kikuu kwa njia ya vinasaba.

Naye Mratibu wa kitengo cha kifua kikuu Zanzibar, Khamis Abubakar, aliitaka jamii kuacha kuwanyanyapaa watu wanaogua kifua kikuu ambao wamegundulika na kuanza matibabu kwa sababu mgonjwa wa kifua kikuu akianza matibabu huwa haambukizi mtu mwingine.

"Ugonjwa huu unaambukiza endapo mgonjwa wa kifua kikuu hajaanza kupata matibabu...lakini niwasisitize wananchi wanapokua na dalili za kifua kikuu kuharakisha hospitali kupata tiba miongoni mwa dalili hizo ni kikohozi ambacho kimechanganyika na damu au kupungua uzito wa mwili," alisema.

## Mariam Mwinyi aipongeza taasisi kwa msaada

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, ameipongeza Taasisi ya Ahmad Mohamed Al Falasi kwa misaada waliyoitoa kwa ajili ya wananchi wenye mahitaji maalum katika kipindi cha kuelekea mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Akipokea misaada hiyo jana ikiwamo vyakula tofauti, mafuta ya kula, tende, mashafu na dawa kwa ajili ya kinamama na watoto huko ofisini kwake Migombani, Mariam alieleza kuwa atahakikisha misaada hiyo inawafikia walengwa.

Mama Mariam Mwinyi ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), aliishukuru na kuipongeza taasisi hiyo kwa misaada iliyoitoa ambayo alisema imekuja wakati muwafaka ambapo wananchi wa Zanzibar wamo katika maandalizi ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Pia taasisi hiyo imeikabidhi Wizara ya Afya msaada huo wa vyakula kwa watendaji pamoja na dawa kwa ajili ya Hospitali ya Mnazimmoja na makabidhiano hayo yalifanyika wizarani na kupokelewa na Waziri wa Afya.

Akizungumza baada ya makabidhiano hayo, Waziri Mazrui, alisema kuwa msaada huo umekuja baada ya kumwomba Mwenyekiti wa Taasisi hiyo kuisaidia Zanzibar katika nyanja mbalimbali.

Alisema dawa zilizotolewa zitasaidia kuongeza lishe kwa wajawazito na watoto ili kuondokana na ugonjwa wa utapiamlo.

Alisema kuwa mwenyekiti wa taasisi hiyo pia anatarajia kujenga hospitali kubwa ya kisasa Zanzibar ili kurahisisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Vile vile, atahakikisha msaada uliotolewa unatumika ulivyotarajiwa ikiwamo vyakula ambavyo vitatolewa kwa watumishi wa wizara hiyo ikiwamo wauguzi na wakunga.

Kwa upande wake kiongozi wa Taasisi hiyo, Sheikh Ahmad Mohamed Al Falasi kutoka Falme za Kiarabu (UAE), alisema kwamba taasisi yake itaendeleza utamaduni huo kuwasaidia wananchi wa Zanzibar ili kuhakikisha wenye mahitaji maalum wanapatiwa misaada hiyo hasa katika kipindi cha kuelekea mwezi wa Ramadhani.

# Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema serikali inaendelea kuchukua hatua za kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kujenga mazingira rafiki kwa wawekezaji.

Aliyasema hayo juzi wakati akizindua wa hafla ya uzinduzi wa kampuni ya mawasiliano ya intaneti Tanzania (Smile) mjini hapo.

Alisema serikali imefanya marekebisho ya sheria mbalimbali na sera hasa kwa kuzingatia bila ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hawataweza kuvutia wawekezaji.

Alisema wanaendelea kutoa vivutio zaidi vya kikodi na visivyo vya kikodi na kuboresha mifumo ambayo itawezesha mamlaka za serikali kutoa uamuzi wa haraka katika utoaji wa vibali vya uwekezaji.

"Tumeshaanza kuona mafanikio makubwa sana katika hili ambapo Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ina uwezo kwa sasa kutoa vibali vya uwekezaji ndani ya saa 48 wakati awali tulikuwa tunatumia miezi mitatu," alisema.

Alisema kuwa kampuni hiyo imekuja muda muafaka na kuipongeza kwa kuwekeza, programu maalum ya kukuza vipaji na kulea vijana waliojikita katika TEHAMA na serikali ipo tayari kufanyakazi kwa pamoja ili kufikia malengo yao.

Alisema sera ya serikali ni uchumi wa bluu na sekta muhimu inayoratibiwa ni TEHAMA na serikali imepanga kuendeleza miji mipya ya kisasa ili kufanikisha uhitaji mkubwa wa kuwa na mindombinu ya kimtandao ambayo ipo imara na kutoa huduma za uhakika.

Naye Mkurugenzi wa kampuni ya Smile, Zuwena Farah, alisema lengo ni kutoa huduma ya kimtandao kwa kasi zaidi na kufikia watu milioni 300 barani Afrika.

Alisema Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imekuwa na mchango mkubwa kuhakikisha wananchi wananufaika na mtandao wenye kasi.

Alisema Smile imewekeza kuboresha huduma na kuzifanya kuwa za kisasa ikizingatia teknolojia ya kisasa, wateja wao wakiendelea kupata huduma bora za kimtandao wenye kasi.

Alisema kampuni hiyo itashirikiana na serikali kutunza mazingira kwa kuboresha teknolojia ya mawasiliano isiyo na uharibifu wowote wala kuhatarisha maisha ya binadamu.



GENEVIEVE UNACHANGANYA WATU Ukurasa.14

JUMAMOSI MACHI 26, 2022

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



## SAA 48 ZIMEPITA

# “Mimi Steve naachia ngazi”

SASA ni wazi kibarua cha msemaji wa Shirisho la Muziki, Steve Nyerere, kipo mashakani baada ya Baraza la Sanaa Tanzania, kuingilia kati kusimamisha uteuzi wake.

Uteuzi wake umeibua kutokuelewana kati ya viongozi wenyewe na wanachama wake ambao wengi hakubaliani nao wakiwa na hoja kwamba hawakushirikishwa.

Baraza limeeeleza hatua hiyo imekuja baada ya kufanya kikao Machi 23 na kuridhia Msemaji huyo kukaa pembeni hadi hapo mgogoro huo utakapopatiwa ufumbuzi.

Katibu Mtendaji wa Basata, Matiko Mniko, amesema uamuzi huo ni hatua nzuri ya kuleta maelewano ili chombo hicho kiweze kufanya kazi zake kama inavyokusudiwa.

Rais wa Shirikisho hilo, Ado Novemba, ndiye anayelaumiwa kwa kuweka baraka zake kwa Steve Nyerere kuchukua nafasi hiyo, ambayo idadi kubwa ya wanachama wanaona kama hafai na hana vigezo vya kufanya kazi katika tasnia hiyo.

Ikumbukwe Steve Nyerere yupo katika sanaa ya filamu na ucheshi, suala ambalo linaonekana ni kichekesho kuteuliwa katika nafasi hiyo kwa sababu hajui chochote kuhusu muziki.

Vinara wa kupinga ni mbunge wa Muheza na mwanamuziki mkongwe Mwana FA, Wakazi, Baba Levo na Whiteness kibonge mwepesi, wote wakiwa na hoja moja kwamba uteuzi huo haukufuata utaratibu.

Awali Mwana FA na Steve Nyerere kila mmoja alimpa mwenzake saa 48 awe amejiuzulu au kuomba radhi.

Hata hivyo, Steve ameonekana kushindwa kucheza karata yake vizuri na hatimaye ndani ya saa hizo 48, ametangaza kujiuzulu na kusema amelazimika kufanya hivyo ili kuleta umoja.

Amesema hana ugomvi wala kinyongo na Mwana FA “Sina kinyongo na Mwana FA, namuomba asiwafikirie vibaya viongozi hawa ili kuleta umoja,” amesema.

Akamalizia “Mimi Steve kwa akili zangu, nimeamua kuachia ngazi naenda kufanya kazi zingine,”

BASI SAWA

## Serikali yawaonya wasanii wakubwa




WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa amewataka viongozi wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) na COSOTA, kuhakikisha wasanii wote wanasajiliwa na akaonya kuwa hakuna masanii mkubwa kama nchi.

Amesema haiwezekani wasanii wakubwa bado hawajajisajili mpaka sasa kitu ambacho kinavunja moyo na kuamuru kuanzia sasa wasanii wote watafutwe na kuingizwa katika usajili ili watambulike.

"Tutaanza kuulizana uwezo wa yule mtu tuliyempa nafasi, hakuna msanii mkubwa kuliko nchi, lazima wasajiliwe na waingie kwenye kusimamia mambo yao ya kimsingi,"

## Sarah asema 'Nikumbushe'



BAADA ya kufanya vizuri na kolabo yake na Martha Mwaipaja, mwimbaji wa injili Sarah Adam, ameachia wimbo mwingine unaoitwa Nikumbushe.

Akizungumza na BT, Sarah amesema wimbo huu unahamasisha jamii kukumbuka walipotoka na kusaidia wahitaji pale ambapo Mungu anakuwa amewabariki.

"Lengo la wimbo ni kumwomba Mungu anikumbushe mimi na wewe tusiwe na kiburi pale tunapokuwa tumefanikiwa, video tayari ipo kwenye channel ya YouTube" amesema.




## Zari hilo haliwezekani kimtazamo

KAULI ya mrembo tajiri kutoka Uganda, Zarina Hassan maarufu kama Zari, imeibua utata baada ya kukiri kulala kitanda kimoja na Diamond Platnumz, bila kugusana.

Zari amefunguka kuhusiana na mahusiano yake ya sasa na Diamond katika kipindi cha "Young African and Famous" amesema wao wamebaki kama wazazi na sio wapenzi.

"Mimi na yeye tuna uhusiano mzuri. Mimi na Diamond tunaweza kulala kitanda kimoja, lakini hakuna kugusana"



## Ivory Coast yaitoa kimasomaso Afrika

AFRIKA imebahatika kutwaa nafasi ya tatu katika shindano la urembo la Miss World lilofanyika nchini Puerto Rico, Jumatano ya wiki hii.

Olivia Yace kutoka Ivory Coast amefanikiwa kushika nafasi hiyo ya tatu, huku mlimbwende wa Poland Karolina Bielawska, akishinda taji la Miss World na nafasi ya pili imekwenda kwa Shree Saini wa Marekani.

Shindano hilo lilitakiwa kufanyika Desemba mwaka jana, lakini lilisogezwa mbele kutokana na baadhi ya washiriki kupata maambukizi ya UVIKO-19.

## Wanamuziki povu tupu

**Na Adam Fungamwango**

WIKI hii hali ilichafuka, baada ya mwigizaji wa filamu mbalimbali, zikiwemo za ucheshi, Steven Mengere, maarufu kama Steve Nyerere kuteuliwa kuwa msemaji wa Shirikisho la Muziki Nchini Tanzania.

Steve ambaye hivi karibuni pia amekuwa akijihusisha na mambo ya siasa, aliteuliwa kuwa msemaji wa shirikisho hilo, chini ya Rais wake Addo Mwasongwe na Katibu Mkuu Fid Q. Hata hivyo uteuzi huo ukawatibua baadhi ya wanamuziki na wasanii ambao waliibuka waziwazi kupinga hilo.

Moja ya madai yao ni kwamba kwamba wanataka kusemewa na mtu anayejua changamoto zao na siyo mtu mwingine ambaye walimtaja kuwa ni mwanasiasa na muigizaji na si mwanamuziki.

Baadhi ya wasanii walipinga katakata uteuzi huo ni Ney wa Mitego, Diamond, Q Chief, Afande Sele, Mwana FA na wengineo wengi. Steve naye akachefukwa, akawaita Waandishi wa Habari na kudai kuwa hawezi kujiuzulu 'kihunihuni', kitu ambacho kilizua mjadala mkubwa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Baraza la Sanaa Tanzania BASATA nalo likapigilia nyundo yake kuwa msemaji huyo kwa kutoa maelekezo kuwa asianze kutekeleza majukumu yake ya nafasi hiyo hadi itakapoamuliwa na Baraza.

Haya ni baadhi ya maneno ambayo baadhi ya wasanii waliyazungumza kutokana na sakata hilo.

**MWANA FA**

Vigezo na utaratibu vimekiukwa na Katiba ya Shirikisho na sisi tunataka ifuatwe. Kama kuna haja ya kuwa na msemaji na yule anayetwaja kwenye katiba, basi tushirikishwe ili tuamue kwa pamoja.

Hata hao viongozi wa Shirikisho ukiwakagua, utagundua kuwa ufanyaji kazi yao ya muziki siyo kwa kiwango kikubwa kama hawa walioko uraiani wa upande wa pili.

**DIAMOND PLATNUMZ**

Mbele ya kamera unatabasamu, ila najua unatabasamu ila unajua kabisa ukikaa peke yako unajuta na kujua kuwa umejivunjia heshima kubwa uliyoijenga kwa muda mrefu. Wewe ni maarufu, usikubali kupoteza heshima uliyoijenga kwa maumivu na jacho kisa mihemko, pasi kutumia fikra.

**FID Q**

Nimepitia maoni yenu kuhusu teuzi ya ndugu Steve. Ni kweli nimehakiki. Nimemuona ana vigezo vya kuwa msemaji wa Shirikisho la Muziki, hivyo basi ninawaomba muwe na imani na subira na kisha tuupe muda fursa ya kutueleza zaidi-Fid Q.

**MWIJAKU**

Huwa mnaitwa kwenye vikao hamtokei, leo wenzenu wamefanya maamuzi mnaanza kukenua midomo. Mngehudhuria vikao vya maamuzi. Nasimama na Steve Nyerere.

**BABA LEVO**

Msanii wa bongo movie, aje kuwa msemaji wa wanamuziki, ni ajabu. Hisia zangu ni kwamba Steve anajuana na baadhi ya viongozi wengi, nadhani lengo lao kwenye kupata 'fungu', lakini kwenye kazi hii sidhani kama anatufaa-Baba Levo.





## Binti Ngoma; muuaji anayejiua mwenyewe

**Na Adam Fungamwango**

USILOLIJUA ni kama usiku wa kiza. Waswahili wanasema hivyo. Ila cha kujifunza ni kwamba akili ya kuambiwa changanya na zako.

"Kuanzia leo, kazi hii ya kuua ndiyo itakuwa shughuli yako, unatakiwa kufanya hivyo ili ulipize kisasi. Wewe ni sawa na kunguru, usiwaze kama ipo siku utarejea kwenu. Ni kwamba huna kwenu. Wewe ni sawa na mbwa mwitu, kula na shibe yako itategemea mawindo yako." Ni maneno mazito anayoambiwa mtoto wa miaka saba tu.

Zubeda, au binti ngoma anaelelewa na babu yake mzee Kigwe. Mzee huyo anamfundisha binti huyo jinsi ya kulenga shabaha kwa bastola.

Alipofikisha umri wa miaka 20, alikuwa ni hatari kwa kutumia bastola. Baada ya kumtia ujasiri, mzee Kigwe alimtayarisha kuanza kulipiza kisasi. Akamwambia binti huyo kuwa baba na mama yake waliuawa na kikundi cha watu fulani kwa sababu fulani, lakini kikubwa zaidi ni kwamba yeye anampa orodha ya wote ambao waliwaua wazazi wake.

Binti huyo mbichi anaanza kuua mtu mmoja baada ya mwingine. Mauji yanaanza kutishia watu kijijini hapo. Mkutano wa wanakijiji unafanyika. Mwenyekiti anaonyesha kushangaa na mauaji hayo, kwani yanafanywa kwa kutumia bastola ambapo ni nadra sana kwa mtu kuwa nayo kijijini hapo. Pia bastola hiyo ni ya aina moja. Ina maana muuaji ni huyo huyo na anatumia bastola hiyo hiyo.

Filamu hii inaitwa 'Binti Ngoma' na baadhi ya wasanii walioicheza ni Abdallah Mtepa na Seif Amini.

Siku moja binti ngoma alikwenda kumuua mmoja wa wanawake wanaotakiwa kuuawa kama orodha inavyosema.

Katika hali ya kushangaza, siku zote alikuwa akivaa kizuia sura, lakini kabla ya kumuua mama huyo aliivua.

Aliyetakiwa kuuawa akashangaa na kumwita jina la Zubeda. Akamuuliza amemjuaje? Akamwambia anamfahamu tangu mdogo na yeye ndiye aliyemlea.

Ndipo mama yule anajifahamisha kuwa yeye alikuwa hausigeli wa mama yake mzazi. Akamwambia kuwa anayeishi naye si babu yake, bali ni baba yake mzazi na si kweli anavyoaminishwa kwamba baba na mama yake wameuawa na watu ambao anawaua kwa kulipiza kisasi.

Mama yule akamwambia baba yake huyo anayemtuma kuua watu, ndiyo aliyemuua mama yake mzazi na kisa ilikuwa ni kung'amua kuwa aliwaua wazazi wake kwa sababu ya mali.

Akamwambia bibi na babu yake mzaa mama waliuawa na mzee Kigwe ili mali zichukuliwe na mkewe ili wazimiliki wote, lakini baadaye alimuua mkewe baada ya kutambua hilo, hivyo mali zikabaki kwake.

# Kylie kwani jina lina tatizo gani?



MWANAMITINDO maarufu wa Marekani, Kylie Jenner, ameibua mjadala mzito baada ya yeye na mume wake Travis Scott kubadilisha jina la mtoto wao aliyezaliwa hivi karibuni.

Katika akaunti yake ya Instagram, Kylie alisema mtoto wao huyo sasa haitwi jina la Wolf, badala yake watu wamuite Fyi.

"FYI ndio jina la mtoto wetu na sio Wolf, tunahitaji awe na furaha ya kweli na imetubidi tuweke wazi kwa sababu kila mtu anamjua kwa jina hilo la zamani," amesema.



## Mary ukisikia rushwa ndio hiyo

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Mary Lazarus, amesema anapata furaha pale anapojikusanyia pesa nyingi kutoka kwa wanasiasa wanaotaka kupigiwa kura.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Mary amesema ana mpango wa kujiandaa na msimu wa mavuno ya pesa katika uchaguzi unaotarajiwa kufanywa nchini humo.


"Kama kila mwanasiasa atanipa pesa ili kumchagua, nitafurahi kukusanya noti. Ni pesa zangu kwa sababu kama akutawala kabla, lakini ni mkono wangu umempigia kura," amesema.

## Yaw Tog awaambia ukweli

RAPA anayekuja kwa kasi nchini Ghana, Yaw Tog, amesema Wanaigeria hawana ukarimu na wanamchukulia msanii kutoka nje ya taifa hilo kama mtu wa kawaida.

Yaw Tog, alihudhuria tuzo za muziki za AFRIMMA mwezi Desemba mwaka jana.

Katika mahojiano yake na redio Y107.9 FM, amesema mapokezi aliyoyapata ni ushahidi tosha kwamba Wanigeria kamwe hawawezi kuwachukulia Waghana kama Davido au Burna.





## Genevieve unachanganya watu

UTATA umeibuka baada ya mwigizaji wa Nollywood, Genevieve Nnaji, kuonyesha dalili ya kubadili dini.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Nnaji ameweka baadhi ya aya za kitabu cha Quran, ikieleza kila nafsi itaonja umauti, swali kabla hujasswaliwa na kisha kuambatanisha na picha yake ambayo inaonekana nywele zake kaziweka kama vazi la hijab.

Ujumbe huo ameutoa siku chache baada ya kutoa ule unaohamasisha upimaji wa afya ya akili kwa kila mtu anayeendelea kuishi.

## Solja Boy kuwa baba lazima utulie

RAPA wa Marekani, DeAndre Cortez Way, maarufu kama Soulja Boy, anatarajia kuwa baba baada ya mpenzi wake Jackie kuwa mjamzito.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, mwanamuziki huyo mwenye vituko lukuki ameweka video akiwa kwenye hafla ya kufurahia ujio wa mtoto wake wa kwanza.

Marafiki na mashabiki zake wamemiminika katika ukurasa wake wakimpongeza kutokana na habari hizo njema na kumsihi kutulia wakati akitarajia kuitwa baba.



UCHAGUZI KENYA 2022

# William Ruto ataweza kuvunja ngome za utatu maarufu Kenya?

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE kengele ya kuanza mbio za kuwania urais katika nchi ya Kenya imesikika, vigogo wanaotaka kuwania nafasi hiyo wanaendelea kuzunguka kila kona kuweka ushawishi wao wapate ridhaa ya wananchi kupitia sanduku la kura.

Macho ya wengi yapo kwa vigogo wanaotawala siasa za nchi hiyo, Rais Uhuru Kenyatta, Raila Odinga na Makamu wa Rais, William Ruto.

Rais Uhuru Kenyatta hawezi kugombea kwa mara ya tatu, lakini turufu yake imekwenda kwa rafiki yake wa sasa Raila Odinga, huku akimtupa chini makamu wake kwa kile anachoeleza hana dira ya kuendeleza nchi hiyo.

Hata hivyo, William Ruto, anazidi kujiimarisha katika siasa za Kenya, kupitia chama chake cha Democratic Alliance United Party (UDA), anataka kuhakikisha anavunja ngome za familia tatu ambazo zinaonekana kuwa vinara wa siasa nchini humo.

Tume ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) imetangaza kuanza rasmi kwa mbio hizo ikiwamo michakato ya kuwachagua wagombea wa urais ambao watashiriki katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Agosti 9, 2022.

Kwa mujibu wa IEBC, vyama vya kisiasa au muungano wa vyama vya kisiasa, vinaweza kushiriki uteuzi wa kuwachagua mgombea kwa moja wa wagombea urais/ naibu rais au kushiriki mchujo wa vyama.

Muda wa kuendesha kura za mchujo kwa vyama au kupitisha uteuzi wa moja kwa moja utaanza Aprili 22 hadi 28, mwaka huu.



William Ruto **PICHA: MTANDAO**

**MISUGUANO ILIYOIMARISHA FAMILIA TATU**

Wachambuzi wa siasa za nchi hiyo wanasema Ruto anatakiwa kufanya kazi ya ziada kung'oa mizizi ya familia ya Kenyatta, Odinga na Moi ambazo zimekuwa zikitawala tangu Kenya ipate uhuru mwaka wa 1963.

Ikumbukwe kwamba Mzee Jomo Kenyatta na Jaramogi Oginga Odinga, walianza kutawala siasa za Kenya hata kabla ya nchi ya Kenya kupata uhuru. Wawili hawa walikuwa viongozi shupavu katika makabila yao.

Kenyatta aliiongoza jamii ya Kikuyu na Odinga aliisimamia vyema jamii ya kabila la Luo.

Wanasiasa hawa wawili walifanya kazi kwa bidii bila woga kuwezesha jamii zao na kuzikinga dhidi ya unyanyasaji wa wakoloni huku wakiwa wamependwa na kutajika katika jamii zao kama viongozi shupavu na wakombozi.

Hata hivyo, mambo yalibadilika baada ya uhuru. Katika kitabu chake, Not yet Uhuru, Odinga anaeleza kuwa kwa Wakenya wengi, uhuru ulikuwa bado haujapatikana kwa sababu mkoloni mpya alikuwa amechukua nafasi ya mwingine.

Kilichofuatia baada ya uhuru ni kujiuzulu kwa Odinga kutoka serikali ya Kenyatta na hatua za kisiasa zilizofuata zilikuwa ni mabishano makali ya kihistoria baina ya familia hizi mbili mashuhuri.

Miaka miwili kabla ya kifo cha Jomo Kenyatta, mnamo Agosti 1978, na baada ya uchaguzi uliokuwa na ushindani mkali wa mwaka wa 1974, kinyang'anyiro kilifikia kilele, huku washindani wakibishana na kutupiana maneno makali kwenye mikutano ya hadhara kuwaonya wananchi wa Kenya dhidi ya hatari za uwezekano wa Daniel Arap Moi kumrithi Jomo Kenyatta.

Kikundi hiki kilitaka katiba kubadilishwa ili makamu wa rais asiwe na uwezo wa kumrithi rais iwapo rais atakufa, mabadiliko ambayo hayangemruhusu Moi kumrithi Jomo Kenyatta.

Moi anatoka kabila la Wakalenjin kutoka Baringo na kikundi kilichofahamika kama "Kiambu Mafia" kilimdharau na hakikuweza kuwaza uwezekano wa Moi kuwa rais wa Kenya.

Baada ya hapo, yeye pamoja na mtoto wake, Raila, walishutumiwa kwa makosa mbalimbali ya uhaini iliyosababisha kutupwa kuzuizini, kuzuiliwa nyumbani, na kupigwa marufuku kuzungumza kwenye hadhara.Hatimaye, Jomo Kenyatta alimteua Daniel Arap Moi kuwa makamu wake na kuonyesha ni nani aliyemtaka kama mrithi.

Moi, aliyetoka kwenye jamii iliyoonekana ndogo alionekana kama chaguo zuri na kama ngazi ya kuleta jamii pamoja baina ya makundi mbali mbali.

Uhusiano baina ya familia ya Odinga na ile ya Kenyatta haukuweza kuwa mzuri kisiasa.

Baada ya Daniel Moi kuchukua hatamu za uongozi aliendeleza sera za Mzee Kenyatta kisiasa na kuitenga familia ya Odinga.

Raila Odinga na babake, Jaramogi, walitajwa kwenye jaribio la kuipindua serikali ya Kenya lililofanyika mwaka wa 1982 ambalo halikufaulu.

Raila alizuiliwa kwa miaka sita bila kufikishwa mahakamani lakini aliachiliwa mwaka wa 1989. Hata hivyo, Raila alifungwa tena karibu mwaka mmoja baadaye pamoja na wakereketwa wengine wa kupigania mfumo wa vyama vingi kama Kenneth Matiba na Charles Rubia.

Hata hivyo, aliachiwa huru mwaka 1991 na akatorokea Norway, akihofia maisha yake.

Baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini Kenya, Raila Odinga alirudi Kenya na kujiunga na Forum for the Restoration of Democracy (FORD, wakati huo ikiongozwa na babake, Oginga Odinga.

Kilichofuata baadaye ni msururu wa kushirikiana kwa vyama, miungano, na kuundwa kwa vyama vipya.

Wakati mmoja, kwa mshangao mkubwa, Raila aliungana na Moi na kuunda chama kipya kilichojulikana kama New Kanu. Hali hii ilipelekea baadhi ya wandani wake, wapinzani na wafuasi sugu kumuita mtu ambaye yuko tayari kulala na shetani ili kufikia lengo lake la kuwa rais wa Kenya.

Kinachobainika katika historia ya siasa za Kenya, wakati wa hatamu za uongozi wa Moi, familia ya Kenyatta haikujishughulisha na siasa; badala yake ilizingatia shughuli za kuunda mtandao wa biashara.

Machi 9, 2018, Rais Uhuru Kenyatta na mpinzani wake, Raila Odinga, waliwashangaza watu baada ya kujitokeza nje ya jengo la Harambee na kutangaza kuweka pembeni uhasama wao wa kisiasa.

Hivi ndivyo Uhuru Kenyatta na Raila Odinga walipoanza ushirikiano wao mpya na kufanya familia zao na ile ya Moi kurudi kuwa zenye nguvu kisiasa.

Baada ya Kenyatta kurudi kwa awamu ya pili katika kiti cha rais, wawili hao walishirikiana kuunda Jopo la Maridhiano (BBI) kwa lengo la kumaliza tatizo la ukabila.

Hata hivyo, Makamu wa Rais William Ruto, aliwekwa pembeni kiasi ambacho alionekana kuwa mpweke na hapo ndipo alipoanza kampeni kubwa ya kuhakikisha kiti hicho kinakwenda kwakwe, tofauti na kiongozi wake Kenyatta, ambaye alionekana dhahiri kutomuunga mkono.

Kuna tetesi kwamba mpango wa mabadiliko ya katiba umetokana na jopo la BBI kumhusisha mtoto wa Moi, Gideon Moi, kuwa makamu wa rais kwenye serikali na baadae kumpokea Odinga atakapomaliza muda wake.

**ATAWEZA KUSHINDANA NAO?**

Ruto anaweza kuangushwa kutokana na kukosa raslimali fedha wakati wa kampeni, kwani familia za Kenyatta na Odinga zina ukwasi wa kifedha. Utajiri huo wa kupindukia umesaidia familia hizi mbili kuendelea kutawala siasa za Kenya.

Hata hivyo, Ruto inaelezwa ana uwezo mkubwa wa kifedha sasa, kiasi ambacho hana wasiwasi na Odinga akiamini atapambana naye kila kona.

Muungano wa Azimio ambao unaongozwa na Raila Odinga na ule wa Kenya Kwanza unaoongozwa na Naibu Rais William Ruto, sasa wanakabiliwa na changamoto ya kumtafuta mgombea mwenza na hapo ndipo utabainika upande gani dhaifu na upi imara.

**UTATA UNAOMKABILI RUTO**

Huu ndio utata wa kisiasa ambao Naibu Rais Ruto anakumbana nao anapoelekea kwenye uchaguzi wa Agosti 2022. Anahitaji kusawazisha masilahi ya kikabila na kikanda ambayo yamekuwa yakiunga mkono azma yake ya urais.

Kwa upande wa muungano mpya wa Azimio la Umoja ambao unawaleta pamoja waliokuwa vinara wakuu wa muungano wa NASA 2017, Mudavadi na Wetangula nani anapata nafasi ya unaibu rais?

Ni lazima tukumbuke kwamba, Ruto amesisitiza wahusika wote wanaofuata imani yake wanahitaji kujiunga na chama chake cha kisiasa, yaani Democratic Alliance United Party (UDA) na hivyo kuingia kwa vinara hawa wawili wa zamani wa NASA wakiwa na vyama vyao vya kisiasa kunafufua mjadala huo.

**(Kwa msaada wa mtandao)**

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOELEKEA...

# 203 magari ya kushangaza, yaliyopendwa na watoto

## •Staili yake ya milango kivutio tosha



**Na Adam Fungamwango**

KAMA kuna magari ambayo yalikuwa vipenzi kwa watoto wengi miaka ya nyuma, basi ni aina ya Peugeot 203,ambayo kwa sasa ni adimu sana kuyaona au hayapo kabisa.

Siyo kwamba watoto walipenda kuyapanda la hasha. Watoto wa miaka kuanzia 1960, 1970 na 1980 wao walipenda kupanda gari yoyote ile ikiwemo kudandia, moja ya michezo ya hatari iliyokuwa ikifanywa na watoto wa zamani, lakini magari haya walipenda kwa kuyaangalia tu jinsi yalivyo na staili yake ya milango inavyofunguka.

Na wala haikuwa watoto peke yao, bali hata watu wazima waliyakodolea macho ya mshangao magari hayo, hasa kama ni mara ya kwanza kuyaona.

Magari hayo yalitengenezwa nchini Ufaransa kati ya mwaka 1948 hadi 1960 na kampuni ya magari ya Peugeot.

Hapa nchini Magari hayo Peugeot 203 yalikuwa maarufu sana na kuwa mengi miaka ya 1960 hadi 1970 na yalianza kuadimika katikati ya miaka ya 1980.

Ni kwa sababu kampuni hiyo ilikuwa ikitoa aina mpya ya magari, hivyo yalianza kuonekana kuwa ni ya kizamani.

Kwa sababu katikati ya miaka ya 1970, yaliingia magari mengine aina ya 404, ambayo nayo yalianza kujichukulia umaarufu mkubwa, na kuonekana ni ya kisasa kwa wakati huo.

Mtu akionekana anamiliki gari hilo, au kuendesha anaangaliwa kwa jicho lingine kwa sababu kwa wakati huo ndiyo magari ghali, mazuri ya kisasa, kama ambavyo leo unavyolijua gari lolote jipya na la kisasa.

Kama vile haitoshi, Peugeot wakatoa tena aina nyingine ya gari wakaiita 504 mwishoni mwa miaka ya 1970, ambalo lilizima kabisa umaarufu wa 404.

Hili sasa watoto wa mjini wakaliita 'nguruwe'. Sijajua ni kwa nini, lakini ni moja kati ya magari maarufu na ya kukumbukwa katika historia ya vyombo hivyo nchini Tanzania.

Yalimilikiwa na watu wachache sana, zikiwemo taasisi chache za kiserikali na kidini.

Sasa turudi kwenye gari letu tunalolizungumzia leo 203. Pamoja na magari yote yaliyotengenezwa na kampuni hiyo kuwa mazuri ya kupendeza, yaliyopendwa na wengi hata kuyatazama kwa macho, lakini 203 lilionekana kivutio.

Kwanza tayari wakati 404 na 504 yanatoka na kutamba, 203 yalikuwa tayari yameshaanza kuadimika.

Lilionekana moja moja tu, na kama ikitokea likafika mtaani, linakuwa kivutio na watoto wengi walikuwa wanaitana, wanajazana ili kushuhudia kile ambacho wanataka kukishuhudia.

Upekee mkubwa na ambacho kiliwapendeza na kuwashangaza watoto ni jinsi milango yake ya mbele inavyofunguka.

Mpaka sasa, magari yote unayoyajua milango hufunguka kulia kwenda kushoto, lakini yenyewe milango ya mbele hufunguka kutoka kushoto kwenda kulia.

Kwa ufafanuzi zaidi ni kwamba hufunguka kutoka mbele kurudi nyuma ya gari, badala ya kutoka nyuma na kufungukia kwa mbele.

Na wala usidhani kuwa hufunguka kama mlango wa 'hiace' ambao ni kama unaserereka, la hasha. Wenyewe unafunguka kama magari mengine ya kawaida, lakini ni kama umegeuzwa, mbele nyuma na nyuma mbele.

Cha ajabu ni kwamba lilivyotengenezwa, ni milango ya mbele tu ndiyo inafunguka hivyo, ila ile ya nyuma inafunguliwa kama kawaida tu ya magari mengine yote unayofahamu.

203 mlango wa dereva na ule mwingine wa upande mwingine wa mbele, ufungukaji wake usio wa kawaida, ndiyo ulikuwa ukiwashangaza wengi na kuwa kivutio.

Kwanza kabisa ukiliona kabla hata haujafunguliwa, utaanza kushangaa kuona komeo lake limekaa kushoto kwa mlango wa mbele, badala ya kulia.

Ukifunguliwa ndiyo kabisa utaona maajabu ambayo hujawahi kuyaona kwenye gari lolote lile. Staili hiyo ndiyo iliwafanya watoto kuyapenda sana magari hayo wakati huo na wakiliona tu, wataanza kulifukuza ili kuona litasimama wapi ili kushuhudia mlango unavyofunguka.

Kuna wakati watoto hata wakitumwa, iwe dukani au popote pale kama wakilikuta gari hilo, basi watasimama kusubiri hadi dereva aje.

Kama akiwa amekwenda dukani mara moja ni heri, lakini kama yuko sehemu ambayo atakaa muda mrefu, basi atawachelewesha kwa sababu wao nia yao kutaka kuona mlango unafunguliwa tu.

Kile kitendo cha kuona mlango unatoka mbele kurudi nyuma, tofauti na magari mengine yote, kwao ilileta burudani, raha, mshangao, kivutio na kichekesho kwa wakati mmoja. Ni kwa sababu hawajazoea kuona hali hiyo kwenye magari mengine.

Picha za makala haya, zinaonyesha uhalisia wa jinsi magari hayo milango yake ya mbele ilivyokuwa inafunguka tofauti na magari mengine, kiasi kwa watoto na wakati mwingine hata watu wazima ililetа mshangao.

Haijulikani mpaka sasa ni kwa sababu gani kampuni hiyo iliamua kufanya hivyo. Ilitaka kuleta kitu tofauti, ilitaka kushangaza watu au tu ni staili. Ni kweli ilishangaza sana na hadi leo imebaki kwenye kumbukumbu ya waliokuwa watoto miaka hiyo ambao kwa sasa ni watu wazima. Ukimtajia magari ya Peugeot 203, ataanza kutabasamu, inawezekana baadaye akacheka. Kisa ni staili tu ya milango ya magari hayo.




**Tuma meseji 0716 350434**

HABARI KIMATAIFA

# MWEZI MMOJA VITA UKRAINE

## •MAJESHI YA RUSSIA YARUDISHWA NYUMA
## •YADAIWA 60% MAKOMBORA HAYAKULENGA



Mwanajeshi wa Ukraine akifurahi baada ya kutwaa tena eneo ambalo lilikaliwa na vikosi vya Russia nje kidogo ya mji wa Kyiv.
**PICHA: Reuters**

MASHAMBULIZI yanayofanywa na vikosi vya Ukraine yamefanikiwa kuwasogeza nyuma wanajeshi wa Russia na kutwaa tena miji iliyodhibitiwa.

Wizara ya Ulinzi ya Uingereza imetoa tathmini yake jana ya kijasusi kuhusu vita nchini Ukraine, ikisema kwamba Ukraine imeweza kutwaa tena miji na maeneo ya ulinzi mashariki mwa mji mkuu, Kyiv kutoka mikono ya vikosi vya Russia.

Tathmini hiyo inasema Ukraine pia imekuwa na baadhi ya mafanikio kuyasukuma majeshi ya Russia nyuma kutoka maeneo waliyokuwa wamechukua kaskazini-magharibi mwa Kyiv.

Uchambuzi wa Uingereza unaongeza kuwa njia za usambazaji za Russia zimepanuliwa kupita kiasi.

**MAKOMBORA YA RUSSIA HAYANA SHABAHA**

Makombora ya Russia yanakabiliwa na kiwango cha juu cha kufeli hadi kufikia asilimia 60, hayo yamesemwa na maofisa wa Marekani ambao majina yao hayakutajwa.

Kushindwa kulenga shabaha kunaweza kusababishwa na chochote, ikiwamo kutokuwa na uwezo wa kurusha vifaa hivyo hadi kulipuka yanapotua .

Kiwango kilichoripotiwa, ambacho hakijathibitishwa mahali pengine, kinaweza kuelezea changamoto ambazo Russia inakabiliwa nazo ni kuongeza kasi katika uvamizi wa mwezi mzima.

Kwa mujibu wa Marekani, Urusi imerusha angalau makombora 1,100 tangu vita hivyo kuanza. Hawajasema ni ngapi zililenga shabaha zao na ikiwa zilifanikiwa kulipuka.

**UKRAINE YADAI KUTEKETEZA MELI YA KIVITA**

Meli ya kivita ya jeshi la wanamaji la Russia iliharibiwa na pia meli nyingine mbili ziliharibiwa katika bandari yenye shughuli nyingi ya Berdyansk, vyanzo vya habari Ukraine vimesema.

Jeshi la Ukraine lilitoa picha hiyo mapema Alhamisi, likidai meli ya Orsk ilipigwa na vikosi vyake.

Maelezo kuhusu kilichosababisha mlipuko na moto ndani ya meli hiyo hayako wazi.

Berdyansk iko magharibi mwa mji uliozingirwa wa Mariupol, uliotekwa siku nne baada ya Russia kuivamia Ukraine.

Wiki iliyopita, Televisheni ya Jeshi la Russia ilipongeza kuwasili kwa Orsk huko Berdyansk kama tukio kuu baada ya kuwa meli ya kwanza ya kivita kutia nanga huko.

Picha zilizochukuliwa kutoka kwa ndege isiyo na rubani na mwandishi wa habari wa runinga ya serikali ya Russia Murad Gazdiev, zilionesha shehena ya kivita ikishushwa kutoka Orsk.

**Katika eneo hilo la Rzesow, ambalo liko umbali wa kilometa 50 kutoka mpakani mwa Ukraine, Biden alikutana na Rais wa Poland, Andrzej Duda, katika sehemu ya safari yake ya dharura barani Ulaya.**

**ZELENSKY AZIDI KUWASIMANGA ULAYA**

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alitoa hotuba yake jana usiku wa manane kwenye mkutano wa kilele wa Baraza la Ulaya mjini Brussels.

Alielezea uharibifu na mauaji ya Russia kwa nchi yake, na akashukuru Ulaya kwa kuungana katika msaada wao kwa Ukraine.

Kisha, kwa mtindo wake wa kusema mambo moja kwa moja, aliwaambia viongozi wa Ulaya kwamba walikuwa wamechelewa sana kuizuia Urusi.

"Mmeweka vikwazo, tunashukuru. Hizi ni hatua zenye nguvu, lakini ilikuwa ni kuchelewa kidogo kulikuwa na nafasi," alisema. Akaongeza kuwa kama kungekuwa na vikwazo vya kuzuia labda Russia isingeingia vitani.

Pia aliashiria bomba la gesi la Nord Stream 2, ambapo alipendekeza ikiwa lingezuiwa mapema, Russia isingeleta shida ya gesi.

Zelensky kisha akaomba mataifa jirani kuidhinisha ombi la Ukraine la kujiunga na EU.

**RUSSIA ITAIBUKA IKIWA DHAIFU**

Russia itajutia uamuzi wake wa kuishambulia Ukraine, hayo ni kulingana na Waziri wa Ulinzi wa Marekani anayehusika na masuala ya sera, Colin Kahl akiwaambia waandishi wa habari juzi.

"Nadhani kuna uhakika wa hali ya juu kwamba Russia itaibuka kutoka Ukraine ikiwa dhaifu kuliko ilivyoingia kwenye mzozo," alisema.

"Itakuwa dhaifu kijeshi, dhaifu kiuchumi, dhaifu kisiasa na kijiografia, na kutengwa zaidi." aliongeza

Alisema Warussia wanakosa shabaha sahihi ya makombora katika mzozo huo wa mwezi mmoja.

Kahl pia alisema kwamba tathmini ya mkakati ujao wa Marekani itaitangaza Russia kama tishio kubwa, lakini akaongeza kuwa nchi hiyo haileti changamoto ya muda mrefu kwa Marekani kama China.

Ulaya umeituhumu Urusi kwa Uhalifu wa kivita nchini Ukraine. Kwa mujibu wa azimio la viongozi wa umoja huo Russia itaadhibiwa kwa kufuata sheria za kimatiafa.

Umoja huo ulisema hayo baada ya mkutano wa kilele uliofanyika nchini Ubelgiji, na kueleza serikali ya nchi hiyo itawajibishwa kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

Azimio la Baraza la Umoja wa Ulaya linasema Russia imekuwa ikiratibu mashambulizi dhidi ya umma wa watu na kuyalenga maeneo ya umma, ikiwamo hospitali, viwanda vya madawa, shule na makazi.

"Kumalizia huo ni uhalifu wa kivita lazima usitishwe mara moja," lilisema azimio hilo.

Wakati huo huo, kundi la mataifa yenye nguvu ya viwanda duniani yaani G7, yameonya dhidi ya kutumika kwa silaha yoyote ya maangamizi dhidi ya Ukraine.

Baada ya mkutano wao wa kilele wa dharura kuhusu uvamizi wa Ukraine, taarifa ya pamoja ya mataifa hayo ilitoa onyo la kutumika kwa silaha za kemikali, bailojia, nyuklia au zozote zenye kufanana na hizo.

Imeitaka Russia kutimiza matakwa ya makubaliano ya kimataifa ya kulinda kila mmoja.

**BIDEN AFANYA ZIARA MPAKANI POLAND NA UKRAINE.**

Katika taarifa yake ya jana Ikulu ya Marekani, imesema Rais Joe Biden, alitembelea nchi ya Poland ambayo inapakana na Ukraine, kwa lengo la kuonyesha mshikamano kwa Ukraine dhidi ya uvamizi wa Russia.

Katika eneo hilo la Rzesow, ambalo liko umbali wa kilometa 50 kutoka mpakani mwa Ukraine, Biden alikutana na Rais wa Poland, Andrzej Duda, katika sehemu ya safari yake ya dharura barani Ulaya.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken alisema katika ziara yake ya Machi 5 alilitembelea eneo hilo kwa lengo la kuonyesha uungaji wake mkono kwa wanajeshi wa NATO, kwa iliyokuwa sehemu ya Jumuiya ya Kisovieti.

Ikulu ya Marekani ilisema katika ziara hiyo ya Ijumaa, Biden alipokea taarifa ya namna gani Poland inakabiliana na wimbi la mamilioni ya wakimbizi ambao wanakimbia makombora ya Russia huko Ukraine.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA TEMEKE**
**MKOA DAR ES SALAAM KITUO CHA JUMUISHI**
**SHAURI LA MADAI/ NDOA NA.../2022**
**JINA LA MDAI MICHAEL FRANCIS MCHWEMBA**
**JINA LA MDAIWA PAULINA BLASUS MTIKATIKA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za mwanzo)**

**kwa PAULINA BLASUS MTIKATIKA**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/ wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 27 mwezi 4 mwaka 2022 saa 3:00 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hutohuduria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati yakuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 23 mwezi 3 mwaka 2022

HAKIMU

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NO.129/2021**
**LITO DAUDI MWAKAPYAMILE..............................MDAI**
**DHIDI YA**
**1.PATRICK PHILIP MWALUSAMBA...................................MDAIWA**
**2.SARAH ANYAMBILILE MWAKIBETA..............................MDAIWA**

**YAH:KUITWA SHAURINI**

**KWA:**
**PATRICK PHILIP MWALUSAMBA NA ANYAMBILILE MWAKIBETA**

Fahamu kwamba **LITO DAUDI MWAKAPYAMILE** amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 28/03/2022 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
**Kumbuka:**Msipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 09/02/2022.

T. Munzerere
MWENYEKITI
09/02/2022.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Baruapepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P 2888,**
**40470 DODOMA**
**Tarehe 25-03-2022**

**TANGAZO**

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAPILI tarehe 27-03-2022 kampuni ya **LOGISTICS FOR SUB SAHARA** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **MTUKULA** kuelekea **TUNDUMA** kupitia **MIKUMI**
**Gari hilo lenye namba za usajili na vipimo vyake**

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**380 SSC FS/HPM 668 FS**
**UREFU 22**
**UPANA 4.00**
**KIMO 4.60**

Gari hilo linatoka MTUKULA kuelekea TUNDUMA kupitia MIKUMI.gari litasafiri muda wa mchana tu
( kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12;00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

---

**IN THE DISTRICT COURT OF TANZANIA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 47 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MARIA JUMANNE HASSAN**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATIX OF A SMALL ESTATE BY MARTHA CONSTANTINE WENGA**
**FORM NO 58**
**APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATIX OF SMALL ESTATE**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN.369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 2 Day of .........5.......... 2022.

Dated at Dodoma this 25 Day of March, 2022.

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KINGLION INVESTMENT COMPANY LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye USAJILI NAMBA **MC249 CGR,** CHASSIS NAMBA **L7GPCKLY3K1015272,** ENGINE NAMBA **KL157FMJ2K5015272.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/122252/2022**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF TANZANIA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.... OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE STEPHANO MASAKA CHISUMBILI**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SAMWEL STEPHANO MASAKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of the Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 26 Day of 04 2022.

Dated at Dodoma this 21st day of March, 2022.

MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**KAHAMA IMPORT AND EXPORT LTD** anatangaza kupotolewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **T.405 BZH** yenye Chassis Na. **LTZHCMLA4B3000072,** Engine Na. **163FMLB0002225,** yenye radi NYEKUNDU.
Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
TAARIFA YA POLISI:
**KAH/ TR/RB/184/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Wilaya ya MUFINDI Kituo cha MAFINGA Mkoa IRINGA Usimazi wa mirathi Na 3/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU KING CHARLES KAGOSE WA MAFINGA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA GRACE VALENTINE SILAYO**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama ya Wilaya ya Mufindi)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowowte/madlahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 Mwezi 02Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimazi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
* Marehemu hakuacha wosia.
* Futa isiyohusika.

Imetolewa leo Tarehe 23 Mwezii 03 Mwaka 2022

HAKIMU MKAZI

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DIGINA KIZUNGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER BM 150** nyeusi yenye USAJILI NAMBA **MC 816 BSL,** CHASSIS NAMBA **MD2A21BYOHWC86283,** INJINI NAMBA **PFZWHC26662.** Kwa yeyote atakaeonekana atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA :
**WMB/RB/231/2022**

---

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB. NA. MG/LD/230464**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: KIBA FARMS AND ENTERPRISES S.L.P 461 MOROGORO.**

**ARDHI: KIWANJA NA. 70 KITALU "E" MSAMVU MANISPAA YA MOROGORO**

**MUOMBAJI: CHARLES OCT AIAN LUGOME S.L.P 6172, MOROGORO.**

Taarifa imetolewa kwamba BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka terehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.

HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO ikionekana, irudishwe kwa MKURUGENZI WA MANISPAA – MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO.

Valency HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA**
**WILAYA YA KIBAHA**

**SHAURI LA ARDHI NA. 07 LA 2022**
- **DAUDI AARON W. KONDORO**
- **BEATRICE NICODEMUS KONDORO............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**
**JUSTINE EMANUEL MAIRA, SCOLASTICA OMBUTU/O ASEWNO, MARIAM SAID KINDAMBA, DANIEL MARTIN LYIMO, KASSIMU MUSTAFA MAHENA & FATUMU MUSTAFA KIKUPA, HADIJA J. HUSEIN, EVA ALOYCE KIMBE, JUMA MRISHO KOMBO, RASHIDI MWINYIHIJA MINJUMA, IBRAHIM MPEYI ALLY, ATHUMANI MAINDA SHABANI, RUKIA RAMADHANI RASHIDI, ANNASTAZIA SAMWEL MTUMBUKA, HIYALI RAJABU SELEMANI, FADHILI YUSUPH & TELFENA SADALA, TWAHA DIHENGA MASIKU, MBWANA KASSIMU MBWANA HADIJA, MUDASIL YAHAYA ALLY, ABEID SHABANI SAIDI, SUBIRA SELEMANI SINGO, DIANA EDWARD MANGWALA...........WAJIBU MAOMBI**
**KWA:**
**JUSTINE EMANUEL MAIRA, SCOLASTICA OMBUTU/O ASEWNO, MARIAM SAID KINDAMBA, DANIEL MARTIN LYIMO, KASSIMU MUSTAFA MAHENA & FATUMU MUSTAFA KIKUPA, EVA ALOYCE KIMBE, JUMA MRISHO KOMBO, RASHIDI MWINYIHIJA MINJUMA, IBRAHIM MPEYI ALLY, ATHUMANI MAINDA SHABANI, RUKIA RAMADHANI RASHIDI, HADIJA J. HUSEIN, ANNASTAZIA SAMWEL MTUMBUKA, HIYALI RAJABU SELEMANI, MBWANA KASSIMU MBWANA HADIJA, MUDASIL YAHAYA ALLY, ABEID SHABANI SAID, SUBIRA SELEMANI SINGO, DIANA EDWARD MANGWALA.**

**POPOTE PALE MLIPO TANZANIA**
Kwa kuwa mleta maombi ameleta shauri la ardhi ambalo limeelezwa katika nyaraka za maombi [Misc Application] ambayo inapatikana katika Baraza La Ardhi na Nyumba [W]-kibaha. Fahamu kuwa shauri limepangwa kutajwa tarehe 04.04.2022 saa tatu asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti Mbuga.
Hivyo mnatakiwa kufika mbele ya Baraza nyinyi wenyewe au mawakili wenu au mtu ambae ameruhusiwa kisheria.
ANGALIA kama hamtohudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Baraza litasikiliza shauri hili na kutoa maamuzi upande mmoja Imetolewa na kutiwa saini na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 08 mwezi Machi, 2022

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA [W]
KIBAHA-PWANI






TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati.

# Operesheni namba moja-**19**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

***DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani.***

***Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati.***

***Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake.***

***Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.***

********************************




Jan alitulia. Alijua Diana analia machozi ya furaha yaliyochanganyikana na uchungu. Uchungu ni kwa sababu ya kutekwa. Hakupata muda wa kulia, kutokana na kuhofia usalama na uhai wake. Moyo wake ukaweka sugu, hivyo alishindwa kulia hadi pale atakaposhuhudia mustakabali wa yote. Machozi ya furaha kwa sababu ameponyeka kutoka kwenye mdomo wa mamba. Alikuwa karibu na kifo zaidi kuliko uhai.

Kwa namna ya ajabu ambayo hakutarajia, si tu kwamba ameokolewa, lakini yupo sehemu salama zaidi. Sehemu anayoipenda kuliko vyote. Yupo na mtu aliyetokea kumpenda. Yupo mikononi mwake. Anahisi joto lake. Hayo yote yakichanganyika, ndipo anapolia machozi ya uchungu iliyochanganyika na furaha.

"Hakuna chochote kibaya kilichokupata tangu umekwenda huko?" Ni swali ambalo alilitegemea, lakini hakulitegemea kwa wakati ule.

"Najua, najua una wasiwasi na wale manyang'au kuwa labda wangeweza kunifanyia chochote. Ingewezekana kama wao ndiyo wangekuwa vinara wa kundi lile. Usichokijua ambacho hata askari nimewapa siri kuwa kinaongozwa na wanawake watatu. Wao wanawatumia wanaume kuwakamata wanawake. Ni wanawake matajiri, lakini kazi yao ndiyo hii. Wanajua ukimkamata mwanamke, inakuwa ni rahisi sana ndugu, mume, mpenzi kutafuta pesa haraka ya kukomboa. Wakiwateka wanawake wanapeleka kwao, kwa hiyo wanakuwa salama. Hawawafanyi chochote. Ila unazabuliwa vibao viwili vitatu siku ambayo unashikishwa simu ili uongee na ndugu zako, kuonekana kuwa kuna mateso sana. Wanachohitaji ni pesa tu, lakini huduma zote chakula, matibabu unapata. Ni watu wazuri, hasa wale wanawake ambao huwezi kuona sura zao kamili." Diana alitiririka na kumpoza Jan ambaye kiasi fulani wivu ulikuwa umeshaanza kumuingia.

"Mpenzi Diana." Sauti ya Jan ilisikika. Haikujulikana kama anaita au analitaja tu. Lakini Diana akaitikia.

"Nimehangaika sana kwenye hili. Nimehatarisha sana maisha yangu. Mimi ndiye niliyekuwa nakwenda kuweka mkoba wa pesa chini ya madaraja. Mwanzo ilikuwa kwa Mfugale, lakini hii mara ya mwisho ni chini ya daraja la Kajima. Nimejitoa muhanga kupigana na watekaji kwa sababu yako. Usinione hivi nimeua watekaji wawili. Nimewasaidia baadhi ya polisi waliokuwa wanataka kuuawa. Nimeona maiti nyingi kwa mara ya kwanza kwenye maisha yangu. Yote hii kwa ajili yako, vinginevyo nisingejisumu kufanya hivyo. Hata hivi sasa najishangaa. Kwa vipi niliweza kufanya vile. Ujasiri ule nimeupata wapi?" Jan alinyamaza baada ya Diana kumgusagusa mgongoni na kuhisi kitu kama shoti ya umeme.

"Pole sana mpenzi wangu, pole."

"Ahsate. Nikwambie tu hata hizi pesa siyo kama zilikuwa zimekamilika shilingi milioni hamsini kama watekaji walivyokuwa wakizitaka. Mjomba alikuwa hana uwezo huo, akawa anahangaika afanye nini. Nikamwambia hilo niachie mimi. Nilijua hata tufanyeje hatuwezi kuzipata. Tungechelewa ungeuawa. Na tungewaambia kuwa hatuna, usingekuwa hai. Nilichofanya ni kwenda kwa Chala na kumuuliza yeye atatoa kiasi gani? Akaniambia atatoa shilingi milioni kumi na tano tu. Na hata baada ya hapo hakujishughulisha tena na hilo, wala kuulizia. Nilichomwambia mjomba ni kwamba asitoe pesa yoyote hizo hizo zinatosha. Aliogopa na kusema wakigundua itakuwa ni hatari, nikamwambia niachie mimi kwa sababu mimi ndiye nitakayepeleka." Alishusha kidogo pumzi. Wakati wote huo walikuwa wamekumbatiana, kila mmoja akiwa na hamu na mwenzake. Hawajaonana muda mrefu. Hakuna aliyekuwa na uhakika kuwa watakutana tena wakiwa hai.

"Nikwambie tu ukweli ni kwamba mle kwenye mkoba niliweka makaratasi badala ya pesa. Niliuchukua mkoba ule niliopewa na mjomba pamoja na zile pesa za Chala, nikaenda nazo nyumbani, nikabadilisha, nikachukua mkoba mwingine uliokuwa umejazwa makaratasi ndiyo niliokuwa naupeleka huko watekaji walikokuwa wanautaka."

"Mhh, sasa wangekuta makaratasi?" Aliuliza Diana kwa sauti laini.

"Ndiyo maana nilikuwa nawahusisha askari licha ya kwamba wenyewe hawakutaka. Nilifanya hivyo kwa sababu kwamba pesa zenyewe hazitoshi, kwa hiyo yote yalikuwa hatari. Hata wangepata idadi hiyo ya pesa wasingekubali. Kwa hiyo nikaona ni bora tu nizichukue, lakini nitumie mbinu za kuhakikisha hawajui hili kwa kuwaita polisi kwenye tukio lao la kuchukua pesa ili wakamatwe." Jan alikuwa akitiririka jinsi alivyopanga mipango yake.

"Sasa askari hawakukuuliza pesa ziko wapi?" Diana aliendelea kuuliza.

"Nimeulizwa swali hilo pale kituoni Magomeni. Nimewaambia mkoba kiukweli haukuwa na pesa kwa sababu hatukuwa na pesa za kuwapa, kwa hiyo tulijaza makaratasi ili waamini kuwa ni kweli, ikiwa tumewekwa mtego wa polisi, vinginevyo ingekuwa balaa."

"Kwa hiyo unazo hizo pesa?"

"Ninazo, tena humu humu ndani, utaziona tu baadaye."

"Huyo mjinga Chala aliyetoa hizo pesa, yeye hajajishughulisha na chochote?

"Labda tukutane naye, halafu umuulize mwenyewe, maana nikisema mimi unaweza kusema najifagilia kwa sababu yeye anakutaka na mimi nakupenda."

"Hivi alidhani pesa ndiyo kila kitu? Ona yeye ametoa pesa halafu amekaa. Na pesa zenyewe hazitoshi, lakini wewe hukuwa na pesa, lakini umefanya maarifa mengi hadi mimi leo hii nimekuwa hai na niko hapa." Diana aliongea kwa hisia kali.

"Yaani afadhali hata marehemu Afande Marco, yeye hakutoa pesa, lakini alijitolea kukusaidia kwa kuwatumia askari polisi wenzake."

"Ni kweli Jan, lakini Marco naye alikuwa anafanya hivyo kwa sababu yeye hiyo pia ni kazi yake. Alikuwa anafanya kitu ambacho kiko kwenye uwezo wake wa kikazi. Ila ni wewe peke yako uliyeonekana umeacha kila kitu na kuamua kwenda na mimi." Diana hakumaliza maneno hayo akaanza kulia tena. Safari hii hakulia machozi ya furaha na uchungu.

Alililia ya uchungu. Alilia kwa sauti ya kwikwi. Jan alimuacha alie. Kuna mtu aliwahi kumwambia mwanamke akilia kwanza muache. Kwa sababu machozi humaliza sumu ya uchungu wote uliomo mwilini. Wanawake wengi wakipatwa na matatizo, uchungu au kuudhiwa hulia.

Na wakimaliza wanamaliza kila kitu. Lakini wanaume wao huona aibu kulia, hasa mbele za watu au hata sirini. Huweka maumivu yao vifuani na mioyoni mwao. Sumu haiondoki, wanaendelea kuugulia miaka na miaka. Ndiyo maana huwa ni wagumu wa kusamehe kuliko wanawake. Mara nyingi huwafanya kutangulia kufa kuliko wanawake.

**Hivi alidhani pesa ndiyo kila kitu? Ona yeye ametoa pesa halafu amekaa. Na pesa zenyewe hazitoshi, lakini wewe hukuwa na pesa, lakini umefanya maarifa mengi hadi mimi leo hii nimekuwa hai na niko hapa.**

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KOCHA DODOMA JIJI AIHOFIA PRISONS

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha wachezaji wa Dodoma Jiji wakianza rasmi mazoezi ya kujiandaa na mechi ya raundi ya 19 ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Prisons, Kocha Mkuu wa timu hiyo Mrundi Masoud Juma ameweka wazi kuwa moja ya kitu ambacho hakipendi ni kucheza dhidi ya timu hiyo.

Akizungumza wakati wa mazoezi ya timu yake kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Masoud amesema kuwa tangu aje Tanzania kwa mara ya kwanza akiwa na klabu ya Simba, huwa wapendi kucheza na timu ya Prisons kwa sababu hutumia zaidi nguvu na wameendelea kucheza hivyo hadi leo, hivyo anaamini mechi hiyo itakuwa ni ngumu kwao.

Dodoma Jiji itasafiri hadi jijini Mbeya kucheza na wajelajela hao kwenye Uwanja wa Sokoine, Aprili 2 mwaka huu.

"Tangu nije Tanzania, sipendi kucheza na timu hiyo. Wanatumia nguvu sana, sipendi sana aina yao ya uchezaji.

Kama walikuwa wakitusumbua Simba wakati huo naifundisha, je kwa timu kama hii Dodoma Jiji? Kwa maana hiyo mechi itakuwa ngumu sana, ukichukulia kwanza hawako kwenye nafasi nzuri kwa hiyo watakuwa wagumu zaidi, kusema kweli itakuwa mechi ngumu sana," alisema Masoud, kocha wa zamani wa Simba.

Alikiri kuwa msimu huu ligi imekuwa ngumu na timu hazijatofautiana sana pointi kwani wao ambao wako kwenye nafasi ya 11, wana pointi na wanazidiwa pointi saba tu na Azam FC ambayo iko kwenye nafasi ya tatu.

"Yaani hapo inaonyesha kuwa timu hazijatofautiana sana pointi, ukishinda leo unapanda juu zaidi, lakini ukipoteza utashuka chini sana, kwa hiyo ni lazima tupambane," alisema kocha huyo.



Kwaya ya Chuo Cha Utumishi wa Umma, ikiburudisha wakati wa uzinduzi wa daraja la Tanzanite jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tukuyu Band yaja na coroca*

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya Tukuyu Sound, imetunga wimbo uitwao 'corona', kwa lengo la kuhamasisha Watanzania kujikinga na ugonjwa huo kwa kwenda vituo vya afya kupata chanjo pia kuzingatia mwongozo wa Wizara ya Afya.

Mmoja wa viongozi wa bendi hiyo, Kalala Junior aliliambia gazeti hili, jijini Dar es Salaam jana kuwa wimbo huo utaanza kufanyiwa mazoezi wiki ijayo na kisha wataingia studio kuurekodi.

Kalala alisema, mara ya kwanza baadhi ya wanamuziki akiwamo yeye, waliungana na kutunga wimbo wa kuhamasisha jamii kuwa makini dhidi ya ugonjwa huo.

"Sasa nasi bendi ya Tukuyu Sound tumeona tuandae wimbo wetu wa kuhusu ugonjwa huo, kwani tunaona kila kukicha unazidi kujiimarisha duniani, hivyo tutajiandaa kuanza mazoezi ya wimbo uitwao 'corona'," alisema Kalala.

Alisema, anaamini watafikisha ujumbe wao kwa jamii iwapo wimbo huo utakamilika ili kila Mtanzania awe makini badala ya kubweteka wakati huu ambao janga la corona linaendelea kutesa dunia.

"Wanamuziki tunaweza kufikisha ujumbe kuhusu corona kupitia maonyesho yetu ya kila mwisho wa wiki lakini pia kwa kurekodi wimbo wetu na kusambaza katika studio ili usikike," alisema.

Alisema, mwongozo wa Wizara ya Afya unaitaka jamii kuchukua hatua ikiwamo kuepuka misingamano isiyo ya lazima, kuvaa barakoa, kutumia vitakasa mikono na kunawa kwa maji tiririka.

"Pamoja na hayo, mwongozo unatuelekeza kutojazana kwenye vyombo vya usafiri kwa ajili ya usalama wetu, hivyo nasi tunaandaa wimbo ukiwa na ujumbe huo muhimu kwa jamii," alisema.

Kalala ambaye pia ni mwimbaji, aliwashauri wanamuziki wa bendi mbalimbali kuangalia uwezekano wa kutunga nyimbo za kuhamasisha vita dhidi ya corona ikiwa ni mchango wao wa kusaidiana na serikali katika vita hiyo.

Alisema, wanamuziki ni sehemu ya jamii, na kwamba hawapaswi kujikita katika nyimbo za mapenzi tu bali waangalie pia na matukio mbalimbali yanayotokea ndani ya jamii na kuuelimisha umma.

## Maandalizi Tanga City Marathon yakamilika

**Na Cheji Bakari,** TANGA

WAKATI kesho Jumapili Machi 27, ndio siku ya mashindano ya riadha ya Tanga City Marathon Season 6, maandalizi yote yamekamilika na jumla ya washiriki 1,500 wakiwemo Wakuu wa Wilaya kutoka mikoa sita nchini wamethibitisha kushiriki mbio hizo.

Muandaaji Mkuu wa mashindano hayo, Juma Mwajasho amesema kuwa hadi kufikia jana, jumla ya tiketi 1,500 zimeuzwa ikiwa ni malengo ya asilimia 100 ya mauzo ya tiketi zote.

Amesema kuwa washiriki hao ni washiriki binafsi, kutoka vyama vya riadha na klabu za jogging kutoka mikoa yote ya Tanzania ikiwemo ya nchi jirani ya Kenya.

"Tunashukuru hadi kufikia leo Ijumaa (jana) tumeuza tiketi zote na washiriki 1,500 wamethibitisha kushiriki mbio hizo wakiwemo Wakuu wa Wilaya kutoka mikoa sita," alisema.

Katika mbio hizo za urefu wa kilometa 21, 10 na 5 ambazo zitazinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima zitaanzia katika viwanja vya jumba la Makumbusho maarufu Tanga Urithi kuzunguka mitaani na kuhitimishwa katika viwanja hivyo.

## Polisi yaitisha Ruvu Shooting

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa timu ya Polisi Tanzania umesema kwa sasa unapeleka akili na nguvu zote kwenye mchezo wao dhidi ya Ruvu Shooting utakaopigwa Aprili mosi mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha msaidizi wa Klabu hiyo alisema wanaendelea na maandalizi kuekelea kwenye mchezo huo.

"Tunaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na timu ya Ruvu Shooting ni mchezo ambao utakuwa na ushindani mkubwa na tunaendelea kujipanga kwa mandalizi," alisema.

Aidha alisema Ligi msimu huu ina ushindani mkubwa, lakini wao watapambana kuhakikisha wanapata pointi tatu katika kila mchezo wa nyumbani.

"Lengo ni kubakiza pointi 3 nyumbani tunaomba mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono."

Alisema michezo ya kirafiki atakayoicheza itawasaidia wachezaji kuwa fiti zaidi kuelekea kwenye mchezo huo.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**LEWANDOWSKI ATAKIWA BARCA**
BARCELONA wanamtaka mshambuliaji wa Bayern Munich na nahodha wa timu ya taifa ya Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33. (***Sport***)

**RAPHINHA AGOMBEWA**
KLABU pia imeungana na Liverpool, Manchester City na Bayern Munich katika mbio za kumsaka winga wa Leeds na Brazil Raphinha mwenye umri wa miaka 25, ambaye anauzwa kwa pauni milioni 60. (***Mirror***)

**ORIGI SOKONI**
MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Divock Origi mwenye umri wa miaka 26 anafanya mazungumzo na wapinzani wa Serie A, AC Milan na Inter Milan kuhusu uwezekano wa uhamisho msimu huu wa joto. (***90min***)

**MITCHELL AFUATILIWA**
KLABU ya Manchester City ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinazomfuatilia beki wa Crystal Palace, Tyrick Mitchell baada ya mchezaji huyo wa miaka 22- kujumuishwa katika timu ya taifa ya England kwa mara ya kwanza. (***Sun***)

**ALONSO AITAKA LALIGA**
MLINZI wa Chelsea, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 31, amesema "angependelea" kucheza tena kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga. Raia huyo wa Hispania aliichezea Real Madrid katika timu ya vijana. (***AS***)

**CESAR NJIA PANDA**
NAHODHA wa Chelsea, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 32 yuko njia panda kati ya kusaini mkataba wa mwaka mmoja na Blues hao ama kukubali ofa ya mwaka mmoja kutoka kwa Barcelona. (***Express***)

**RUDIGER HUYO JUVE**
MCHEZAJI wa kimataifa wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 29, anaweza kuwa beki wa tatu wa Chelsea kuondoka Stamford Bridge mkataba wake unapoelekea kumalizika msimu wa joto na tayari amepewa mkataba na Juventus. (***Sky Sports***)

**DIAZ ANYATIWA**
MSHAMBULIAJI wa Blackburn Rovers na Chile, Ben Brereton Diaz mwenye umri wa miaka 22 ananyatiwa na Sevilla. (***Estadio Deportivo***)

**NUNEZ AWANIWA TENA**
KLABU ya West Ham huenda wakajaribu tena kumnunua mshambuliaji wa Benfica na Uruguay, Darwin Nunez, baada ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22 kukataa dau la pauni milioni 50 la kuvunja rekodi ya klabu hiyo Januari. (***Standard***)

**KENT ATAKIWA LEEDS**
LEEDS United inataka kumsajili winga, Ryan Kent kutoka Rangers, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 akiwa na kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 20 katika mkataba wake. (***Football Insider***)

**SPENCE AGOMBEWA**
ARSENAL na Tottenham watahitaji kulipa pauni milioni 20 kumsajili beki wa Middlesbrough, Djed Spence, ambaye mchezo wake huko Nottingham Forest kwa mkopo unaridhisha. (***Express***)

**TRINCAO AWINDWA**
KLABU za Benfica na Sporting Lisbon zinapania kumnunua winga wa Barcelona, Francisco Trincao, ikiwa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22 anayechezea Wolves kwa mkopo hatajiunga na klabu hiyo kwa mkataba wa kudumu wa pauni milioni 25. (***Record***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# JORGINHO: KUKOSA PENALTI KUTANITESA MAISHA YOTE

**Ni baada ya Italia kushindwa kufuzu kombe la Dunia nchini Qatar, sasa watashuhudia mashindano hayo kideoni tu...**

**PALERMO,** ITALIA

JORGINHO amekiri kwamba, kukosa penalti zake mapema kwenye kampeni zitamtesa sana baada ya Italia kushindwa kufuzu kwa Kombe la Dunia la mwaka huu 2022.

Azzurri walitawazwa mabingwa wa Euro 2020 miezi nane tu iliyopita baada ya kuifunga England kwenye fainali kwa mikwaju ya penalti.

Hata hivyo, kikosi hicho cha Roberto Mancini hakitakuwa kwenye Kombe la Dunia baadaye mwaka huu baada ya kufungwa 1-0 na Macedonia Kaskazini kwenye mchezo wa mchujo.

Ingawa wenyeji walitawala mchezo pale Palermo, Aleksandar Trajkovski alifunga dakika za lala salama na kuwapa wageni ushindi wa kushangaza.

Wakiwa wametoka sare mara nne kati ya michezo mitano iliyopita, Italia ililazimika kuingia kwenye mchezo wa mchujo baada ya kumaliza kwa pointi mbili nyuma ya Uswizi katika Kundi C.

**Miongoni mwao kulikuwa na sare ya 1-1 na Uswisi, ambapo Jorginho alikosa penalti mbili ambazo zinge wafanya Azzurri kuwaon doa wapinzani wao kileleni.**

Na kiungo wa kati wa Chelsea alifichua hisia zake za kuwajibika kwa taifa lake kushindwa kufuzu.

"Ni vigumu kueleza kilichotokea," aliambia RAI Sport. "Inauma sana. Nitasema kweli, bado siamini.

"Sidhani tulikosa ubunifu, kwani mara zote tulitawala mechi na kutengeneza nafasi nyingi. Kwa bahati mbaya, hatukuweza kuzimaliza.

"Tulicheza mpira mzuri, tulishinda ubingwa wa Ulaya msimu uliopita, lakini kwa bahati mbaya katika mechi chache zilizopita, tulifanya makosa madogo.

"Inauma ninapofikiria juu ya (penalti nilizokosa), kwa sababu bado ninafikiria juu yake, na itanisumbua maisha yangu yote.

"Kupanda pale mara mbili na kutoweza kuisaidia timu yako na nchi yako ni jambo ambalo nitaendelea nalo milele, na linanielemea.

"Watu wanasema tunahitaji kuinua vichwa vyetu na kuendelea, lakini ni ngumu."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,065

MECHI KALI
ENGLAND
VERSUS
SWITZERLAND
1 | 1.81
X | 3.33
2 | 4.83

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BALE ATUPA KIJEMBE REAL MADRID




**CARDIFF,** Wales

GARETH Bale alielezea kukosolewa kwake kama mchezaji wa Real Madrid ni kwa "kuchukiza" baada ya kuiongoza Wales katika ushindi kwenye mechi za mchujo wa kufuzu kombe la Dunia.

Bale amecheza katika mechi tano pekee kati ya 42 za Madrid katika mashindano yote msimu huu, jumla ya dakika 270 uwanjani - sawa na mechi tatu nzima.

Akiwa amewahi kuwa mchezaji ghali zaidi katika soka duniani, winga huyo hakuwepo kwenye mechi ya hivi majuzi zaidi ya Madrid, wakati wakipokea kipigo kichungu cha mabao 4-0 kutoka kwa wapinzani wao Barcelona.

Hata hivyo, Bale alikuwa amereja katika ubora wake wakati Wales wakipata ushindi Alhamisi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alikuwa nahodha wakati nchi yake ikipata ushindi wa 2-1 dhidi ya Austria, akifunga mabao mawili - la kwanza kwa mkwaju wa faulo.

Mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham alionekana kufurahia sherehe hizo, lakini sauti yake ilibadilika kidogo alipoulizwa kama alikuwa na ujumbe kwa wakosoaji wake nchini Hispania.

"Hapana," aliiambia Sky Sports. "Sihitaji kutuma ujumbe, kusema ukweli. Ni kupoteza muda wangu. "Inachukiza, wote wanapaswa kujionea aibu."

## Pedri amuita Haaland Barca




**BARCELONA,** Hispania

PEDRI amemtaka Erling Haaland ajiunge na Barcelona atakapoondoka kule Borussia Dortmund.

Mkataba wa Haaland na Dortmund hautaisha hadi mwaka 2024, lakini inasemekana ana kifungu cha kutolewa ambacho kinamaanisha kuwa anaweza kusainiwa kwa euro milioni 75 mwishoni mwa msimu huu.

Barca, Real Madrid, Manchester City na Manchester United zote zimehusishwa katika nia ya kutaka kumnunua mshambuliaji huyo wa Norway.

Haaland amefunga mabao 80 katika mechi 82 katika mashindano yote ya Dortmund tangu ajiunge nayo kutoka Salzburg Januari 2020, akishinda tuzo ya Golden Boy mwaka huo.

Rekodi hiyo kubwa ya mabao ndio sababu kuu ya Pedri - ambaye aliitwaa Golden Boy 2021 - anatumaini kwamba hatua inayofuata ya Haaland ni kutua Camp Nou.

"Ni kitu kwa klabu. Lakini Haaland ana sifa nzuri na karibu kila kitu anachogusa kinaishia golini," alisema Pedri akiiambia TVE.

"Natumai anaweza kuja kwa sababu nimekuwa nikisema nataka wachezaji bora zaidi Barca."

5,872,000

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/03/2022 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Cambridge Utd | 2.29 | 3.29 | 2.95 |
| 02. 26/03/2022 | 18:00 | Airdrieonians vs Cove Rangers | 2.73 | 3.27 | 2.42 |
| 03. 26/03/2022 | 18:00 | Elgin City vs Edinburgh City | 2.42 | 3.20 | 2.67 |
| 04. 26/03/2022 | 18:00 | Peterhead vs Falkirk FC | 2.78 | 3.32 | 2.35 |
| 05. 26/03/2022 | 18:00 | Leyton Orient vs Barrow | 2.24 | 3.29 | 3.04 |
| 06. 26/03/2022 | 18:00 | Carlisle vs Bristol Rovers | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 07. 26/03/2022 | 18:00 | Colchester vs Tranmere | 2.40 | 3.28 | 2.79 |
| 08. 26/03/2022 | 18:00 | Bradford City vs Newport | 2.56 | 3.20 | 2.66 |
| 09. 26/03/2022 | 18:30 | Den Bosch vs VVV Venlo | 2.36 | 3.72 | 2.55 |
| 10. 26/03/2022 | 19:00 | Finland vs Iceland | 2.28 | 3.15 | 3.30 |
| 11. 27/03/2022 | 15:00 | Mirandes vs Ponferradina | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 12. 27/03/2022 | 17:00 | Burgos vs Tenerife | 3.05 | 3.00 | 2.39 |
| 13. 27/03/2022 | 19:15 | Malaga vs Huesca | 2.49 | 3.08 | 2.83 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 26/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1156 | Wisla Pulawy vs Sokol Ostroda | 1.62 | 3.84 | 4.47 |
| 16:00 | 2952 | Osnabruck vs Eintracht Braunschweig | 2.15 | 3.32 | 3.18 |
| 16:00 | 4320 | KamAZ vs Akron Tolyatti | 2.24 | 3.06 | 3.06 |
| 17:00 | 1624 | Croatia vs Slovenia | 1.56 | 3.85 | 6.28 |
| 17:00 | 2733 | Urozhay Krasnodar vs Baltika Kaliningrad | 3.51 | 3.26 | 1.97 |
| 18:00 | 1106 | Doncaster vs Charlton | 3.78 | 3.43 | 1.91 |
| 18:00 | 1155 | Hamilton vs Queen of South | 1.81 | 3.42 | 4.16 |
| 18:00 | 1239 | Bradford City vs Newport | 2.68 | 3.22 | 2.53 |
| 18:00 | 1512 | Annan Athletic vs Albion Rovers | 1.82 | 3.64 | 3.64 |
| 18:00 | 1614 | Scunthorpe vs Harrogate | 3.47 | 3.27 | 2.05 |
| 18:00 | 1788 | Dungannon Swifts vs Crusaders Belfast | 7.58 | 4.86 | 1.31 |
| 18:00 | 1934 | Kilmarnock vs Partick Thisle | 1.80 | 3.41 | 4.25 |
| 18:00 | 2032 | East Fife vs Alloa Athletic | 2.48 | 3.42 | 2.57 |
| 18:00 | 2543 | Airdrieonians vs Cove Rangers | 2.76 | 3.31 | 2.38 |
| 18:00 | 2610 | Kings Lynn vs Halifax | 4.45 | 3.66 | 1.70 |
| 18:00 | 2623 | Northampton vs Hartlepool | 2.09 | 3.21 | 3.46 |
| 18:00 | 2710 | Dumbarton vs Montrose | 3.44 | 3.35 | 2.02 |
| 18:00 | 2714 | Coleraine FC vs Glenavon | 1.83 | 3.45 | 3.79 |
| 18:00 | 2728 | AFC Wimbledon vs Cambridge Utd | 2.29 | 3.32 | 2.92 |
| 18:00 | 2791 | Salford City vs Walsall | 2.09 | 3.22 | 3.42 |
| 18:00 | 2982 | Forfar Athletic vs Cowdenbeath | 1.52 | 3.97 | 5.23 |
| 18:00 | 3203 | Peterhead vs Falkirk FC | 2.76 | 3.35 | 2.36 |
| 18:00 | 3295 | Inverness vs Dunfermline | 1.99 | 3.25 | 3.64 |
| 18:00 | 3656 | Exeter vs Stevenage | 1.69 | 3.62 | 4.76 |
| 18:00 | 3736 | Oldham vs Mansfield | 3.62 | 3.48 | 1.94 |
| 18:00 | 3978 | Kelty Hearts FC vs Stenhousemuir | 1.43 | 4.28 | 6.02 |
| 18:00 | 4272 | Elgin City vs Edinburgh City | 2.53 | 3.16 | 2.58 |
| 18:00 | 4625 | Stirling vs Stranraer | 2.12 | 3.36 | 3.02 |
| 18:00 | 4680 | Ipswich vs Plymouth | 1.89 | 3.46 | 3.81 |
| 18:00 | 4714 | Shrewsbury vs Lincoln | 2.01 | 3.27 | 3.61 |
| 18:00 | 4736 | Queens Park vs Clyde | 1.49 | 4.15 | 5.73 |
| 18:00 | 5296 | Arbroath vs Raith Rovers | 2.07 | 3.20 | 3.45 |
| 18:00 | 5356 | Eibar vs Lugo | 1.59 | 3.61 | 5.73 |
| 18:00 | 5432 | Leyton Orient vs Barrow | 2.08 | 3.27 | 3.42 |
| 18:00 | 5533 | Morton vs Ayr United | 2.27 | 3.06 | 3.16 |
| 18:00 | 5556 | Accrington vs Gillingham | 1.73 | 3.62 | 4.46 |
| 18:00 | 5736 | Port Vale vs Sutton United | 1.98 | 3.27 | 3.71 |
| 18:00 | 5932 | Sheffield Wed vs Cheltenham | 1.53 | 3.95 | 5.73 |
| 18:00 | 5962 | Carlisle vs Bristol Rovers | 2.83 | 3.23 | 2.40 |
| 18:30 | 5115 | Den Bosch vs VVV Venlo | 2.85 | 3.44 | 2.25 |
| 19:00 | 3337 | Finland vs Iceland | 2.30 | 3.13 | 3.28 |
| 19:30 | 3283 | Renate vs Giana Erminio | 1.81 | 3.45 | 4.40 |
| 20:00 | 4141 | Ireland vs Belgium | 5.84 | 3.78 | 1.60 |
| 20:00 | 5294 | Sporting Gijon vs FC Cartagena | 2.15 | 3.28 | 3.23 |
| 20:30 | 5627 | England vs Switzerland | 1.81 | 3.33 | 4.83 |
| 20:45 | 1402 | SBV Excelsior vs Helmond Sport | 1.32 | 5.33 | 7.10 |
| 21:45 | 4854 | Spain vs Albania | 1.15 | 7.07 | 20.19 |
| 22:45 | 2930 | Netherlands vs Denmark | 1.92 | 3.43 | 4.04 |
| 22:45 | 3020 | Germany vs Israel | 1.13 | 7.93 | 20.26 |
| 23:30 | 5902 | Real Oviedo vs Fuenlabrada | 1.79 | 3.22 | 4.76 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KASEKE HAJAKATA TAMAA YANGA

**Na Dennis Fussi**

KIUNGO mshambuliaji wa Yanga, Deus Kaseke amesema pamoja na kukosa nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza, lakini anaamini bado ana uwezo wa kuisaidia timu hiyo.

Kaseke ambaye alitokea Mbeya City hana nafasi kwenye kikosi cha sasa cha Yanga ambacho kimesheheni nyota wengi na hivyo kumfanya kukosa nafasi ya kucheza mara kwa mara.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam, mchezaji huyo amesema anatambua maboresho yaliyofanywa na yanayotarajiwa kufanywa, lakini hilo haliwezi kumkatisha tamaa atazidi kupambana kupigania nafasi yake uwanjani.**

"Kocha ndio mwenye kujua mchango na uwezo wa kila mchezaji, na ukizingatia timu ina wachezaji wengi hatuwezi kucheza wote lazima tupishane," amesema Kaseke.

Kaseke ndio mchezaji pekee aliyebakia kwenye kikosi cha Yanga kilichobeba ubingwa wa mwisho wa ligi kuu ya Tanzania bara msimu wa 2016/17.



Wanawake wa kikundi cha ngoma za asili cha Tabata Women Tapo wakitoa burudani katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Tabata Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waogeleaji 100 kuwania medali

**Na Dennis Fussi**

WAOGELEAJI 100 watachuana kuanzia leo kuwania medali na mataji katika mashindano ya klabu bingwa ya mchezo wa kuogelea yaliyopangwa kufanyika kwenye bwawa la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika jijini Dar es Salaam.

Waogeleaji hao wanatoka katika klabu saba ambazo ni Taliss-IST, Dar es Salaam Swimming Club, Bluefins, FK Blue Marlins, Moshi, Morogoro International School (Mis Piranhas) na Mwanza Swimming Club.

Mwenyekiti wa Kamati ya maandalizi wa Chama Cha Kuogelea Tanzania (TSA), Hadija Shebe alisema kuwa mashindano hayo yamepangwa kuanza saa 2.00 asubuhi na waogeleaji watashindana katika staili tano ambazo ni Freestyle, Breaststroke, Butterfly, Backstroke na Individual Medley.

Kwa mujibu wa Hadija, waogeleaji hao pia watashindana katika relay katika mashindano ambayo yatatumia sheria za Shirikisho la Mchezo wa kuogelea Duniani (FINA) na pia yatatumika kuchagua timu za Taifa kwa ajili ya kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Alisema Tanzania inatarajia kushiriki katika mashindano ya Dunia, Jumuiya ya Madola, mashindano ya Afrika kwa waogeleaji wakubwa na vijana.


"Mashindano haya ni makubwa kabisa kwani hata waogeleaji wa Tanzania wanaoogelea nje ya nchi wamekuja kushiriki. Ni mashindano pekee ambayo yanatumiwa na TSA kuchagua wachezaji wa timu ya Taifa," alisema Hadija.

"Tunatarajia kuona ushindania mkali kwa waogeleaji wetu ili kutafuta nafasi ya kufuzu mashindano ya dunia. Waogeleaji wengi wapo katika maandalizi ya mwisho mwisho kwa ajili ya mashindano hayo, bado tunahitaji wadhamini wa mashindano haya."

Michezo

Jumamosi Machi 26, 2022

Nipashe




Bale atupa kijembe Real Madrid UKURASA 22



Nahodha wa timu ya taifa ya Italia, Ciro Immobile (kulia) akichuana na Stefan Risovski wa North Macedonia wakati wa mchezo baina ya timu hizo mbili wa mchujo wa kufuzu kombe la Dunia nchini Qatar mwaka huu kwenye uwanja wa Renzo Barbera mjini Palermo. Italia ilifungwa bao 1-0 na kutolewa kwenye mashindano hayo. **PICHA: MTANDAO**

# WACHEZAJI SITA MTEGONI SIMBA

## Mikataba yao yafikia ukingoni, maamuzi ya kuongezewa yako chini ya kocha Pablo huku wawili...

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI sita wa Simba wanatarajia kumaliza mikataba yao kwenye klabu hiyo huku kuendelea kubaki au kutobaki kutatokana na ripoti ya Kocha Mkuu, Pablo Franco.

**Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa wachezaji Bernard Morrison, Chris Mugalu, Meddie Kagere, Thadeo Lwanga, Joash Onyango na Paschal Wawa mikataba yao inaelekea ukingoni, huku ikitajwa klabu ipo kwenye mazungumza na baadhi ya wachezaji ambao inataka kuwabakisha.**

"Tunajua kuna baadhi ya wachezaji wanakaribia kumaliza mikataba yao, lakini tuko kwenye mazungumzo nao, na kubaki au kutoendelea pia kutatokana na ripoti ya mwalimu," alisema Meneja Habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally.

Hata hivyo, wachezaji Mugalu na Wawa ndiyo kwa kiasi kikubwa wanaonekana huenda wakaonyeshwa mlango wa kutokea kupisha wachezaji wengine wa kigeni kusajiliwa.

Wawa ambaye msimu uliopita nusura aachwe, aliongezwa mkataba wa mwaka mmoja, huku Mugalu akionekana kuwa zaidi kwenye chumba cha matibabu badala ya uwanjani.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Bodi ya klabu, Salim Abdallah 'Try Again', alisema kuwa watasajili wachezaji wanne wa kigeni wenye uwezo wa hali ya juu, ili kukiboresha kikosi hicho na kuwa imara kwenye msimu ujao wa michuano ya kimataifa.

Alisema wanatarajia kusajili beki mmoja wa kati, mastraika wawili na winga mmoja.

Pamoja na kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho la Afrika hatua ya makundi, lakini baadhi ya wanachama na mashabiki wamekuwa hawaridhishwi na kiwango cha timu hiyo msimu huu.

Wamekuwa wakidai baadhi ya wachezaji wageni na wazawa viwango vyao vimepungua, hivyo kunahitajika usajili wa nguvu kwa ajili ya msimu ujao wa ligi, kuirudisha Simba ile ambayo imezoeleka kuwa tishio kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Baadhi ya wachezaji wanaotajwa kufikia mahali pazuri kwenye usajili ni Victorien Adebayor anayeichezea US Gendamarie ya Niger na Moses Phiri anayechezea Zanaco ya Zambia.

# Yanga haipoi, yaiita Mafunzo

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI timu zipo kwenye mapumziko ya kalenda ya Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), kikosi cha Yanga kitakuwa dimbani Jumatano ijayo Machi 30 kucheza dhidi ya Mafunzo ya Zanzibar.

Mechi hiyo ya kirafiki inatarajiwa kuchezwa kuanzia saa moja usiku kwa saa za Afrika Mashariki kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema kuwa lengo la mechi hiyo ni kuwafanya wachezaji waendelee kuwa na utimamu wa mwili kwa ajili ya kujiweka sawa na mwendelezo wa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ni kweli tuna mechi moja ya kirafiki Machi 30 dhidi ya Mafunzo. Ni hiyo tu kwa sasa, hakuna nyingine, ila kama kutakuwa na mechi nyingine baada ya hapo tutawajulisha," alisema Bumbuli.

Amekanusha tetesi kuwa timu hiyo itakuwa na mechi nyingine ya kirafiki dhidi ya KMC.

Kulikuwa na taarifa kuwa baada ya mechi hiyo, Yanga itacheza mechi nyingine dhidi ya KMC.

"Hilo kwa sasa halipo, nimesikia hizo tetesi na nimekuwa nikiulizwa sana, lakini si kweli, mechi hiyo hiyo moja tu dhidi ya Mafunzo, kama kutakuwa na nyingine basi tutawaambia au mtaona kwenye akaunti yetu kwenye mitandao ya kijamii," alisema Bumbuli.

Kwa kipindi hiki, baadhi ya timu za Ligi Kuu zimewapa wachezaji wake mapumziko, zingine zimekwishaanza mazoezi, zingine zikiandaa mechi za kirafiki, lakini timu kama Namungo yenyewe ipo nchini Zambia kwenye mechi kadhaa za kirafiki kwa ajili kujiweka sawa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >